

5 FEBRUARI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA PILI

Kikao cha Nane – Tarehe 5 Februari, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE

Mhe. Silyvestry Francis Koka

(Mbunge aliyetajwa hapo juu aliapa Kiapo cha Uaminifu na kutoa tamko la Ahadi ya Uzalendo)

SPIKA: Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Stephano Luhende.

5 FEBRUARI, 2026

Na. 127

Uhitaji wa Shule ya Kidato cha Tano na Sita - Bukene

MHE. JOHN S. LUHENDE aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Shule ya Kidato cha Tano na Sita katika Jimbo la Bukene?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025 Serikali imetoa shilingi bilioni 1.4, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika Shule za Sekondari Kili na Mwangoye za Jimbo la Bukene, ili kuzipandisha hadhi kuwa na wanafunzi wa Kidato cha Tano na cha Sita.

Mheshimiwa Spika, Shule za Kili na Mwangoye kwa sasa zina jumla ya wanafunzi 456. Wanafunzi 433 wapo katika Shule ya Kili na wanafunzi 23 wapo katika Shule ya Sekondari Mwangoye. Serikali itaendelea kujenga shule mpya za kidato cha tano na cha sita, hasa za wavulana, au kupandisha hadhi shule zilizopo kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Luhende.

MHE. JOHN S. LUHENDE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii, na pia ninamshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Ni lini sasa Serikali itaona

5 FEBRUARI, 2026

umuhimu wa kuweka masomo ya sayansi kwenye hizo shule za Mwangoye pamoja na ile ya Kili pale Bukene?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ni lini Serikali itamaliza tatizo la madawati katika shule zote za msingi pamoja na sekondari katika Jimbo la Bukene? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa John Stephano Luhende, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ni lini Serikali itaanzisha mikondo ya masomo ya sayansi kwenye shule hizi mbili; Shule ya Kili na Mwangoye, ni kwamba, Serikali kadiri ambavyo inaendelea kuimarisha miundombinu katika shule hii, tutafikia wakati wa kuanzisha mikondo ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, kwa Mkoa mzima wa Tabora, tunayo shule yetu ya kimkoa ya sayansi ya wasichana. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa TAMISEMI, nimwelekeze Afisa Elimu Mkoa, watoto wetu wa Bukene wanapofaulu kwenye masomo haya ya sayansi wapangiwe na wapewe kipaumbele kwenye shule yetu ya kimkoa ya sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilifanya ziara kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwenye huu Mkoa wa Tabora. Serikali tumetoa maelekezo kwenye Serikali yetu ya Mkoa wa Tabora kushirikiana na TFS pamoja na Wakurugenzi, ili kuhakikisha tunaondoa tatizo la madawati kwenye shule zetu zote za msingi na sekondari ndani ya mkoa huo. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Deo Mwanyika.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Njombe tuna shule za sekondari tatu ambazo ziko tayari

5 FEBRUARI, 2026

kuongezwa kwenda kidato cha tano na cha sita kwa sababu zina facility za kutosha; Shule ya Mgola, Shule ya Mpechi na Shule ya Maheve. Serikali ina mpango gani kufanya jambo hilo? Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO): Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kupandisha hadhi Shule za Sekondari kwenda kuwa za kidato cha tano na sita kwa kadiri ya mipango iliyopo ndani ya dira yetu kwa kadiri tulivyoipitisha hapa.

SPIKA: Waheshimiwa, kutokana na ratiba ya leo, tutakuwa na uchaguzi ambao utatuchukua zaidi ya saa tatu. Hivyo tutakuwa na swali la nyongeza moja moja tu. Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas. (Makofi)

Na. 128

Mradi wa Bonde la Mto Msimbazi

MHE. TARIMBA G. ABBAS auliza:-

Je, lini Mradi wa Bonde la Mto Msimbazi utanza na kukamilika?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tarimba Abbas Gulam, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Bonde la Mto Msimbazi unalenga kupunguza athari za mafuriko katika eneo la Jangwani na kuboresha mipango miji katika eneo la chini la bonde. Mradi ulianza kutekelezwa rasmi mwezi Februari, 2023 na utatekelezwa kwa muda wa miaka sita

5 FEBRUARI, 2026

awamu kwa awamu. Mradi unatarajia kuhamisha nyumba zaidi ya 3,000 ambapo hadi sasa nyumba zaidi 2,500 zimeshalipwa fidia na kuhama eneo la mradi.

Mheshimiwa Spika, mradi unatarajia kupanua na kuongeza kina cha Mto Msimbazi pamoja na kuongeza uwezo wa mawanda ya mafuriko katika eneo la chini la bonde. Udongo utakaotokana na upanuzi huo, utatumika kutengeneza eneo salama kwa makazi na biashara pembezoni mwa Bonde hilo la Msimbazi.

Mheshimiwa Spika, jumla ya hekta 57 zinatarajiwa kupatikana kwa matumizi hayo. Mkataba wa ujenzi huu unatarajiwa kusainiwa mwezi Februari, kwa maana ya mwezi huu, na kazi kuanza rasmi ifikapo mwezi Mei, 2026.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Bonde la Mto Msimbazi unajenga daraja jipya eneo la Jangwani lenye urefu wa mita 390 chini ya usimamizi wa TANROADS. Kazi hii imeanza tangu mwezi Mei, 2025 na ujenzi upo 15%. Mradi utajenga karakana mpya ya mabasi ya mwendokasi katika eneo la Ubungo Maziwa. Mkataba wa kazi hii unatarajiwa kusainiwa mwezi huu wa Februari.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mradi unatarajia kuboresha maeneo korofi katika eneo la juu la Bonde pamoja na kuratibu shughuli za kibinadamu ili kudhibiti mmomonyoko wa udongo unaotua eneo la chini na kusababisha mafuriko.

SPIKA: Mheshimiwa Gulam Abbas.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Mradi ule ulianza kuzungumzwa miaka mitano iliyopita na ni kipindi kirefu sana. Sasa tukiongeza miaka sita mingine, maana yake ni wananchi wa maeneo yale ambayo wanapata sana mafuriko, wanakwenda kupata shida. Swali ni kwamba, Serikali haioni haja ya ku-revise program zake ili kuweza kuharakisha kumalizika kwa mradi huu?

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ni lini wale wenye nyumba zilizobakia, ambao hawajapata fidia, watakwenda kulipwa fidia zao? Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO): Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge kwamba, Mradi huu wa Bonde la Msimbazi ni mradi mkubwa, ni mradi unaogharimu Dola za Marekani karibu milioni 260 ambazo ni Fedha za Kitanzania zaidi ya shilingi bilioni 650. Kwa ukubwa wa mradi huu, ndiyo maana utekelezaji wake unachukua muda mrefu, siyo kwa sababu ya tatizo la fedha; fedha zipo kwenye mradi huu, isipokuwa zile *process* za kukamilisha mradi ndiyo zinafanya tuchukue mradi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tutaanza kwa kuongeza kina cha Mto Msimbazi, kutanua kingo na kuzijenga upya na kutanua zaidi mawanda ya maeneo ya mafuriko, na vilevile kutengeneza hili eneo salama kwa ajili ya makazi na biashara, eneo la ukubwa wa hekta 57. Siyo hivyo tu, mradi huu una sehemu ya utunzaji wa mazingira kwenye eneo la juu la Bonde la Mto Msimbazi, kwa maana ya Misituta ya Pugu pamoja na Kazimzumbwi. Kwa hiyo, ni mradi mkubwa ndiyo maana unachukua muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia kwenye mradi huu, kaya zinazoguswa, kwa sababu zinaguswa na mafuriko, eneo hili la Msimbazi ni 2,775. Tulivyoenda kufanya upembuzi na kuanza ujenzi tumebaini zitaongezeka kaya nyingine 314 ambazo hazikuwa kwenye mpango wa awali. Kwenye kaya zile za mpango wa awali, kaya 2,775 tayari Serikali imeshalipa fidia kwa kaya 2,602 na zile zilizobaki, zimebaki siyo kwa sababu Serikali haina fedha, ni kwa sababu, familia zenyewe zinakuwa zina mambo kadhaa ya kisheria ama ya kuelewana au ya kimazingira.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Hasunga.

5 FEBRUARI, 2026

Na. 129

Ujenzi wa Soko la Mazao la Kimataifa

MHE. JAPHET N. HASUNGA aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Soko la Mazao la Kimataifa katika eneo la Tacri Mbimba utaanza?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mbunge wa Vwawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kujenga soko la kisasa pamoja na stendi mpya katika Eneo la Mbimba katika Mji wa Vwawa. Aidha, mradi huu utahusisha matengenezo ya barabara kwa kiwango cha lami kwa urefu wa kilomita 8.8. Miji yote 18 ya kundi hili kwenye huu Mradi wa *TACTIC*, ukiwemo Mji wa Vwawa, utekelezaji upo hatua ya usanifu. Utaratibu wa kutangaza zabuni utaanza baada ya kupata Mkandarasi na washauri wasimamizi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Hasunga.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri sana ya swali hili. Maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, usanifu bado haujakamilika. Je, ni lini sasa usanifu huu utakamilika ili soko hili lianze kujengwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, wananchi wa Mji wa Vwawa wamekuwa wakipata shida sana katika kuuza mazao yao ambayo wamekuwa wanayazalisha kwa wingi sana, lakini wafanyabiasha kutoka nje wamekuwa wakienda hadi mashambani

5 FEBRUARI, 2026

na kununua kwa bei za chini sana. Ipi Kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba, sasa hivi wanaweza kuruhusiwa kuanza kuuza mazao yao, kama Soko la Kimataifa, wakati wakisubiri ujenzi wa soko hilo? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO): Mheshimiwa Spika, kwenye awamu hii ya tatu ya utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC*, usanifu kwenye maeneo yote ya Miji 18 utakamilika mwezi huu wa Pili. Baada ya hapo tutakwenda hatua za kutangaza zabuni kupata wakandarasi na washauri wasimamizi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi wa Vwawa kuruhusiwa kuanza kuuza mazao kwenye soko hilo la Kimataifa, naomba niseme kwamba, suala hili ni mtambuka na sisi ndani ya Serikali, TAMISEMI, tunahitaji kushirikiana na wenzetu wa Wizara Kilimo ili kuweza kutoa kauli ya pamoja. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Serikali iliahidi kujenga Mradi wa Soko la Kimataifa kwenye eneo la Mji wa Kalema ambako kumejengwa Bandari, ikiwa ni mradi wa kimkakati. Je, Serikali mpaka sasa ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi huu, na yapata miaka saba toka ilipotoa ahadi hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO): Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na uchambuzi wa miradi yote ambayo tumepanga kuifanya ndani ya dira hii ya miaka 25. Serikali itakapopata fedha na pindi mradi huu utakapopitishwa kwenye mpango wetu wa miaka mitano na mwaka mmoja mmoja hatimaye, kwa ajili ya kutengewa bajeti tutakwenda kujenga soko hilo pale Kalema mara moja.

5 FEBRUARI, 2026

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Devotha.

Na. 130

Mafunzo na Ufuatiliaji wa Miradi

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA aliuliza:-

Je, Serikali imeweka utaratibu gani kwa vikundi vinavyopata mikopo ya Halmashauri kupatiwa mafunzo ya usimamizi ili kuongeza ufanisi?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Daniel.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, samahani, naomba utulivu ndani ya Bunge tafadhali.

Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Daniel Mburarugaba, Mbunge wa Viti Maalum na Mbunge wa Mkoa mzima wa Kagera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeweka utaratibu wa kutoa mafunzo ya biashara kwa wanufaika wa mikopo ya 10% kwa lengo la kuhakikisha mikopo hiyo inatumika kibiashara, kwa tija na kwa uendelevu. Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Vikundi vya Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu za mwaka 2025 zinawataka

5 FEBRUARI, 2026

wanavikundi kupata mafunzo ya ujasiriamali; na Mwongozo wa Utoaji na Usimamizi wa Mikopo unaeleza kuwa, vikundi vipate mafunzo ya siku sita ndani ya wiki sita kabla ya kupata mkopo na kuendelea kutoa mafunzo baada ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuongeza maarifa, ujuzi na mitazamo chanya ya ujasiriamali ili waweze kuanzisha na kuendesha biashara endelevu, kuongeza kipato na kuboresha maisha yao. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imeandaa kitini cha wawezeshaji na wanufaika ili kurahisisha zaidi utoaji wa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Januari, 2026 jumla ya vikundi 24,064 vimepatiwa mafunzo kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Devotha.

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri, kwa maslahi mapana ya Mkoa wa Kagera na pia vijana na walemavu. Ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kabisa kwamba Mkoa wa Kagera ni Mkoa ambao jiografia yake haijaka vizuri. Pia tunafahamu kwamba Maafisa Maendeleo wamepewa majukumu kwa ajili ya kuwasaidia makundi haya kwa kuwasajili kwenye mfumo ili waweze kupata mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuhakikisha hawa Maafisa Maendeleo wanapata vitendeakazi ikiwemo suala la *internet*, kwani wanawake hawa wakienda kuomba mikopo hii mara nyingi wanaambiwa *internet* ipo chini, hatuna uwezo wa *internet*, Serikali imejipanga vipi kwenye suala hili?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Tunafahamu kabisa kwamba mikopo mingi ya walemavu imekuwa ikibaki kwenye

5 FEBRUARI, 2026

Halmashauri kwa sababu walemavu hawa wamepata shida kwenye utambuzi. Je, tutafanyaje ili hawa walemavu nao washiriki kikamilifu? Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO): Mheshimiwa Spika, hivi sasa hali ilivyo, kila mwaka na kila *quarter* tunapopeleka fedha za OC kwenye mikoa yetu na kwenye Halmashauri zetu, tumekuwa tukitenga fedha na kupeleka fedha kwa ajili ya kuwawezesha Maafisa Maendeleo ya Jamii wetu ili waweze kuwafikia wananchi wengi kwenye vikundi, waweze kununua mabando kwa ajili ya kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali katika kujenga mkongo wa mawasiliano kwa Taifa letu kwa ajili ya kuhakikisha kila maeneo yanafikika kwa mtandao kwa maana ya *internet*. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na jitihada hizi na pindi nchi nzima itakapokuwa *covered* na mkongo wa Taifa na kufikika kimawasiliano kwa maana ya *internet* watu wote wataweza kuwa wanafikiwa, lakini kwa sasa tunaendelea na utaratibu tulionao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu walemavu, Serikali inatambua umuhimu wa kundi hili na ndiyo maana katika mikopo hii ya 10%, asilimia mbili imetengwa maalum kwa ajili ya kundi hili. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa TAMISEMI, kuwaelekeza Wakurugenzi wote nchi nzima, kwenye Halmashauri zote 184, pindi wanapopokea maombi ya kundi hili maalum, kundi la walemavu wayachukulie kwa umakini na wawafuate mahali walipo, wasingoje wafuatwe kwenye ofisi zao.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri

5 FEBRUARI, 2026

aliyoyatoa Naibu Waziri, ninaomba niongeze vitu viwili kwa ridhaa yako.

Mheshimiwa Spika, moja, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, tumeanza kuwanunulia pikipiki Maafisa hawa wa Maendeleo ya Jamii. Katika mwaka huu 2025/2026 tayari tumenunua pikipiki 98 na tumeshazigawa kwenye Halmashauri 98 na tunaendelea na zoezi hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu walemavu, tumeshawaelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri zote, kwamba wafanye *inventory* na kujua tunao walemavu wangapi kwenye kila Halmashauri ili wakati tunapowa-*encourage*, kwa sababu ndiyo eneo pekee ambalo hatupati maombi mengi, tunapowapeleka hao Maafisa Maendeleo ya Jamii waweze kufanya kazi kwa urahisi kwa wale walemavu ambao wamekuwa *identified*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea kwa Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Anne Kilango kwa niaba Mheshimiwa Zuena Bushiri.

Na. 131

Kuboresha Umwagiliaji kwenye Kilimo cha Tangawizi

MHE. ZUENA A. BUSHIRI K.n.y. MHE. ANNE K. MALECELA aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka wataalam kwa wakulima wa tangawizi, Tarafa ya Mamba Vunta na Gonja ili kuboresha umwagiliaji?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha uendelevu wa miradi ya umwagiliaji nchini, katika mwaka 2025/2026, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kutoa mafunzo kuhusu uendeshaji,

5 FEBRUARI, 2026

usimamizi na matunzo ya skimu za umwagiliaji pamoja na mbinu za kilimo bora kwa wakulima nchini.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 15 Februari, 2026 Wataalam wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji wataanza kutoa mafunzo kwa wakulima wa zao la Tangawizi katika Skimu za Mamba Myamba, Kihurio, Kwa Sita na Chemchem kwa lengo la kuchangia ongezeko la tija na uzalishaji pamoja na pato la mkulima.

SPIKA: Mheshimiwa Bushiri.

MHE. ZUENA A. BUSHIRI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza wananchi wa Mamba Vunta wanaishukuru Serikali kwa kupokea shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya miundombinu ya umwagiliaji. Swali ni kwamba, kwa kuwa kumekuwana changamoto kubwa kwa mkandarasi, kazi anayoifanya inaonekana kwamba ipo chini ya kiwango. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kutuma wataalam ili kwenda kukagua kazi hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Tarafa ya Mamba Vunta, na Tarafa ya Gonja imekuwa na mwamko mkubwa sana wa kilimo cha tangawizi. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuwasaidia kupeleka miundombinu katika tarafa hizi mbili ili kunyanyua uchumi wa wananchi.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Moja, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali zuri ninajua ni Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Kilimanjaro na anafanya kazi njema.

Mheshimiwa Spika, ninamthibitishia tu kwamba moja, nitatuma timu ya wataalam kutoka Tume, watakwenda kukagua huo mradi na kutuletea majibu na kuhakikisha wanachukua hatua katika yale yote ambayo wananchi watakuwa wameeleza katika eneo hilo.

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu kupeleka miundombinu katika Tarafa ya Mamba Vunta pamoja na Gonja ni wajibu wa Serikali kufanya hivyo, na kwenyewe tutakuja, tutafanya tathmini ili kuendelea kuongeza miradi ya umwagiliaji ili iweze kuleta tija kwa wananchi wa Jimbo la Same Mashariki na Magharibi vilevile na wananchi wote wa eneo hilo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, hakuna swali la nyongeza. Mheshimiwa Baraka Ulimboka.

Na. 132

**Miradi ya Umwagiliaji Mbuga ya Tenende
na Katumba – Songwe**

MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO aliuliza: -

Je, lini miradi ya umwagiliaji ya Mbuga ya Tenende na Katumba - Songwe itaanza?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2025/2026 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi ya umwagiliaji ya Tenende na Katumba – Songwe, kwa ajili ya kujua gharama halisi za ujenzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi hiyo unatarajiwa kukamilika ifikapo Julai, 2026 na hivyo kujumuishwa kwenye mpangokazi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

SPIKA: Mheshimiwa Ulimboka.

MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, katika Wilaya ya Kyela, kuna mradi wa umwagiliaji ambao tayari tunaishukuru Serikali imempa mkandarasi na anaenda vizuri, nimpongeze mkandarasi

5 FEBRUARI, 2026

mzawa anayefanya ile kazi. Je, ni lini skimu hiyo itakamilika kwa sababu kuna changamoto ndogo ndogo zinazomkabili mkandarasi huyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuongozana na wataalam wake kuitembelea ile skimu ili ajue changamoto ambazo zipo nje ya zile ambazo zinaonekana katika nyaraka, kuna baadhi ya maeneo ambayo wananchi wanalalamikia baadhi ya mambo katika fidia?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mbunge wa Kyela, kaka yangu Mheshimiwa Baraka Mwamengo ameanza kazi vizuri, jambo moja tu awe na uhakika nalo ni kwamba, skimu itaisha kwa wakati kwa sababu tutajitahidi kusukuma fedha, vilevile kuhakikisha kwamba mkandarasi anafanya kazi kwa viwango ambavyo tumekubaliana kimkataba. Kwa hiyo, hilo tutapambana nalo ili wananchi wa Kyela waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Nipo tayari, tutaongozana mimi na yeye, bahati nzuri tupo njia moja, nitafika katika hilo eneo pamoja na wataalam, ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Awack.

MHE. DANIEL A. TLEMAI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Je, katika Bonde la Eyasi Serikali ilipeleka shilingi bilioni 38,500, mpaka sasa ni takribani miaka minne mradi ule unaendelea kusuasua. Nini majibu ya Serikali, katika mradi wa shilingi bilioni 38 katika Bonde la Eyasi ambalo Naibu Waziri ni shahidi tuliweza kufika kipindi fulani?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi wa Bonde la Eyasi wenye thamani ya shilingi bilioni 21.6 ni sehemu ya miradi ambayo Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji tunaitekeleza, na

5 FEBRUARI, 2026

tumepeleka kiwango cha fedha na bado tutaendelea kupeleka, changamoto kidogo inayochelewesha tu ni kwamba fedha zinakwenda kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kadri fedha tutakapokuwa tunaendelea kuipata na kuipeleka, tutahakikisha ule mradi unakamilika kama ambavyo tumekubaliana na mkandarasi. Ahsante.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid.

Na. 133

Matumizi ya Vyanzo vya Umeme vya Upepo na Jua

MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia vyanzo vya umeme wa upepo na jua vilivyopo nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Nishati.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NISHATI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nishati, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

SPIKA: Mheshimiwa Waziri ni swali Namba 133 la Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, wewe unasoma Namba134.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, Mbunge wa Mwera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2015 imeweka mkazo wa kuendeleza vyanzo vya nishati

5 FEBRUARI, 2026

jadidifu hususan upepo na jua ili kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na nafuu kupitia vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kutimiza azma hii, Serikali imeshabainisha na kufanya utafiti wa maeneo mbalimbali yanayofaa kuendelezwa kwa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia upepo na jua, ikiwa ni pamoja na Zuzu - Dodoma, Same - Kilimanjaro na Manyoni – Singida. Uendelezaji wa maeneo hayo kwa kushirikiana na sekta binafsi upo katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika kwa sasa Serikali inatekeleza mradi wa kuzalisha umeme wa Megawati 150 katika Wilaya ya Kishapu - Shinyanga, ambapo awamu ya kwanza ya mradi huo yenye Megawati 50 umekamilika, na hatua za kuingiza umeme huo katika gridi ya Taifa zimeanza.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za kuboresha mazingira ya uwekezaji wa sekta binafsi katika vyanzo vya nishati jadidifu (jua, upepo, jotoardhi na vyanzo vingine), Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuboresha mikataba kifani ya kuzalisha na kuuziana umeme.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Suleiman.

MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, moja kati ya mwelekeo wa Serikali yetu ya awamu ya sita ni kwamba ifikapo mwaka 2030 tuweze kuwa na Megawati 8,000 wakati sasa tupo katika Megawati 4,000.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa pia, uwekezaji wa umeme wa jua na umeme wa upepo ni nafuu zaidi kuliko umeme wa *hydropower* pamoja na gesi, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza maeneo mengi zaidi ili ifikapo 2030 tuweze kuwa na Megawati 8,000 kama ni dhamira ya Rais.

5 FEBRUARI, 2026

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mbunge wa Mwera kwa kufuatilia kwa karibu uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali ili kuweza kuweka uimara katika *grid* yetu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango, kwanza inakaribisha wawekezaji mbalimbali ili kuwekeza katika vyanzo tofauti tofauti vya umeme. Pia Serikali inaendelea kufanya uzalishaji wa umeme wa jua kule Shinyanga, Dodoma, Same na Singida, tunazalisha Megawati 715.

Mheshimiwa Spika, umeme wa upepo, Singida pia Makambako na Njombe ipo miradi inaendelea. Jotoardhi Songwe na Ngozi miradi inaendelea na hatua hizi zipo mbalimbali kwenye hatua za utafiti, uwekezaji na maridhiano ya kuuziana umeme kwa TANESCO, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Asha Amani. Hayupo!

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Esther Edwin Malleko.

MHE. ASHA HUSSEIN SALEH: Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Mheshimiwa Esther Malleko.

Na. 134

Usambazaji wa Umeme kwenye Vitongoji Vilivyobakia Kilimanjaro

MHE. ESTHER E. MALLEKO aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza usambazaji wa umeme kwenye vitongoji vyote vilivyobaki Mkoani Kilimanjaro?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu: -

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Deo Ndejemi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko Mbunge wa Viti maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inaendelea na kazi za utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika Mkoa wa Kilimanjaro, ambapo hadi kufikia Januari, 2026, jumla ya vitongoji 2,032 kati ya 2,258 sawa na 90% vilipatiwa umeme na kusalia na vitongoji 226 ambavyo vitapelekewa umeme kupitia miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kati ya vitongoji hivyo, vitongoji 40 vitafikishiwa miundombinu ya umeme kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini Awamu ya Pili A (*Hamlet Electrification Phase IIA – HEP IIA*) na vitongoji 186 kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vitongojini Awamu ya Pili B (*Hamlet Electrification Project Phase IIB – HEP IIB*). Kukamilika kwa miradi hii kutawezesha kufikisha umeme katika vitongoji vyote 2,258 vya Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Malleko.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini nilikuwa na swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya umeme hasa hizi nguzo zimekuwa nyingi, zinaoza na kuanguka, hivyo kusababisha upotevu wa umeme au kukatikakatika kwa umeme kwa maeneo mengi. Nini mkakati wa Serikali sasa kuhakikisha inabadilisha nguzo hizo na kuwa za zege?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi kumjibu Mheshimiwa Esther Malleko. Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Malleko amekuwa anafuatilia kwa karibu

5 FEBRUARI, 2026

namna ya kupeleka nishati na kuwasogezea hasa wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, upo mkakati kupitia shirika letu la umeme TANESCO kuhakikisha tunabadilisha nguzo zote za miti na kuweka nguzo za zege kwa kadri ambavyo bajeti inapatikana. Ninakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, Mji wa Tarime una mitaa ambayo baadhi ina sifa za kama vitongoji, kwa maana ina sifa ya kupata umeme kupitia *peri urban electrification*. Ninataka kujua ile mitaa yote ambayo haina umeme, ni mkakati gani wa Serikali kuhakikisha unapeleka umeme?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, upo mkakati kupitia TANESCO kwa ajili ya kujaziliza kwenye mitaa ambayo ilibaki haikupatiwa umeme. Pia tunao mkakati wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote ambavyo vimebaki havijapatiwa umeme nchini. Ninakushukuru.

SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood.

Na. 135

Mradi wa Maji wa Bilioni 185 Morogoro

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD aliuliza: -

Je, lini mradi mkubwa wa Maji wa Bilioni 185 utaanza Morogoro ikizingatiwa kuwa Morogoro kuna kero kubwa ya maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa usambazaji majisafi na salama kwa ajili ya Manispaa ya Morogoro kwa gharama ya shilingi bilioni 220.8. Miongoni mwa kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa mtambo wa kutibu na kuzalisha maji (*water treatment plant*) lita milioni 54 kwa siku utakaojengwa eneo la Mafiga. Mkataba wa ujenzi wa mtambo huo ulisainiwa tarehe 19 Januari, 2026 na utatekelezwa kwa muda wa miezi 24.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kingo za Bwawa la Mindu unaolenga kuongeza kina cha bwawa kwa mita 2.5, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 372, na ujenzi wa matanki manne (4) yatakayokuwa na uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni tisa yatakaojengwa katika maeneo ya Lukobe, Bigwa, Kiperu na Magereza.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za manunuzi ya wakandarasi watakaofanya kazi mbalimbali zilizobaki katika mradi huo.

SPIKA: Mheshimiwa Abood.

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kuhusu tatizo kubwa la maji katika Manispaa na Morogoro. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Bwawa la Mindu limezungukwa na kaya za kata mbili na zimefanyiwa tathmini. Ili waweze kuondoka wanatakiwa walipwe fidia, lakini hadi leo hii hawajalipwa fidia. Fidia yenyewe inategemea ni kwa bilioni 9.2.

(a) Je, ni lini Serikali italipa fidia ili wananchi wapishe ujenzi wa Bwawa la Mindu ili wananchi waondokane na kero za maji Manispaa ya Morogoro?

5 FEBRUARI, 2026

(b) Je, ni lini Serikali itakamilisha taratibu za manunuzi ya wakandarasi watakaofanya kazi mbalimbali zilizobakia katika mradi huu wa shilingi bilioni 220?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kushirikiana na Wizara ya Maji na kwa kuendelea kutoa *feedback* ya kile kinachendelea katika jimbo lake na kuwatetea wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Serikali inatarajia kulipa shilingi bilioni 9.167 kwa ajili ya fidia ya wananchi hao ambao wamegawanywa katika makundi mawili. Kuna kundi la kwanza ambalo wako ndani ya mita 500 ambapo baada ya kukamilisha uthamini ni shilingi bilioni 4.8 ambazo zitalipwa kwa wananchi hao. Baada ya hapo, kuna utanuzi wa kingo za lile tuta na penyewe linainuliwa kwa 2.5, malipo yake ni zaidi ya shilingi bilioni 4.367.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa majedwali ya mahitaji ya malipo ya fidia haya yako Wizara ya Fedha kwa ajili ya taratibu za malipo, na baada ya kukamilika, wananchi watakuwa wameshalipwa fidia zao. Tumepanga kuwa ndani ya mwaka huu wa fedha wananchi wote wanaoathirika na Bwawa la Mindu watakuwa wamelipwa fidia zao wote.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu mchakato wa kupata mkandarasi. Mchakato huo unafuata sheria na kanuni. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kuwa tutahakikisha kwamba mchakato huu unakwenda kwa haraka ili tupate mkandarasi sahihi kwa ajili ya kutekeleza miradi hii. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Suma.

MHE. SUMA I. FYANDOMO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa swali dogo la nyongeza. Kata ya Mpuguso iliyopo Wilaya ya Rungwe kuna mradi wa kujenga tenki la maji ulioanza mwaka 2023, mpaka sasa haujakamilika. Mradi huo ni wa muhimu sana kwa vijiji vifuatavyo: Kijiji cha Kasyeto, Mbumbuli, Segera, Mbuguso, Isajilo,

5 FEBRUARI, 2026

Mibura pamoja na Kata jirani ya Ilima. Je, ni lini mradi huo wa maji utakamilika, kwani wananchi wa vijiji hivyo wanapata shida sana ya kupata maji?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Fyandomo, Mbunge wa Mkoa wa Mbeya kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Nimtoe hofu, tunayo miradi 878 ambayo tunaendelea kuitekeleza. Ni maelekezo ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kuwa kabla hatujaanza kutekeleza miradi mipya, miradi viporo yote tunaikamilisha, na baada ya hapo sasa tuone matokeo na wananchi waweze kufurahia majisafi na salama katika mabomba hayo.

SPIKA: Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Na. 136

Kufanya Biashara Pembezoni mwa Barabara Kilombero

MHE. ABUBAKARI D. ASENKA aliuliza: -

Je, utaratibu gani wafuate Wananchi wanaofanya biashara pembezoni mwa Barabara za *TANROADS* hususan maeneo ya Mkambe, Kidatu na Mkula?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima, jengo hili limejengwa kwa namna kwamba hata ukizungumza kwa kunong'oneza lina *amplify*. Kama mnavyoliona ndivyo lilivyojengwa. Sasa mkizungumza hata kwa sauti za chini chini, hapa jengo zima hili linakuwa haliendani na taratibu za Kibunge. Hapa Katibu wa Bunge amefunga mtambo wa *voice identification*, kila anayezungumza, mimi ninamwona hapa. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Waziri.

5 FEBRUARI, 2026

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Matumizi ya Barabara za Mwaka 2025, Kanuni ya 36(4) imeweka utaratibu kwa ajili ya wafanyabiashara wenye nia ya kutumia maeneo yaliyopo pembezoni mwa barabara.

Mheshimiwa Spika, Kanuni zinaelekeza kuwa, mfanyabiashara anayetaka kupanga katika hifadhi ya barabara atajaza fomu maalum ya maombi inayotolewa na Wakala wa Barabara Tanzania, *TANROADS* na atatakiwa kulipa ada ya maombi kabla ya kuwasilisha fomu hiyo. Wakala baada ya kupokea maombi hayo itayachakata, na yale yatakayokidhi vigezo *TANROADS* itatoa kibali na kumjulisha mwombaji gharama atakazopaswa kulipia kwa mujibu wa sheria.

SPIKA: Mheshimiwa Asenga.

MHE. ABUBAKARI D. ASENKA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, na tutafuata utaratibu huo ili wananchi wetu waishi kwa utulivu. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Katika barabara hiyo hiyo ya Ifakara - Kidatu bado una wananchi wanadai fidia ya barabara hiyo, na tayari alielekeza Kamati ya Wilaya ifanye kazi yake, na imemaliza kazi yake. Je, ni lini watalipwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mwaka 2024 Mheshimiwa Rais alisimama katika barabara hiyo hiyo ambako tulitoa maombi ya taa za barabarani na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi wakati huo aliahidi. Je, ni lini taa hizo zitafungwa katika barabara hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kuwa fidia ilishalipwa, ndiyo maana kuna utaratibu kwamba baada ya fidia kunakuwa na wananchi ambao kama walipunjwa ama hawakupata kwa bahati mbaya, ama walirukwa, ndiyo maana kamati inaundwa

5 FEBRUARI, 2026

chini ya Mkuu wa Wilaya ili kuweza kusikiliza yale malalamiko ya wananchi. Baada ya hapo ni kuwasilisha hayo maombi ama tathmini hiyo iliyofanyika ili tuweze kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kuyapokea malalamiko hayo ya wananchi ambao hawakulipwa, Serikali inayafanyia kazi na wananchi hao watalipwa baada ya pia Serikali kujiridhisha kwamba kweli hawa watu wanastahili kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la taa, tuna utaratibu ambao umewekwa kabisa kwamba kwa sasa barabara zote ambazo ni mpya ikiwepo na hiyo barabara ya Mheshimiwa Asenga, maeneo yote ambayo yamekuwa kama miji yatawekewa taa za barabarani.

SPIKA: Mheshimiwa Sigrada Mligo.

MHE. SIGRADA W. MLIGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Swali langu ni kwamba kuna barabara ya Njombe – Ludewa maarufu kama Itoni – Lusitu, ni miaka miwili na nusu sasa imesimama, na hata ilipoleta shida juzi wametafuta mkandarasi wa ndani. Je, Serikali ina kauli gani kuhusu mkandarasi mwenye mkataba huo?

Mheshimiwa Spika, pia Mhandisi Mshauri wa mradi huo mpaka sasa anaishi hotelini, hana nyumba ya kuishi. Je, Serikali ina kauli gani kwa leo kuhusu barabara ya Itoni – Lusitu, Njombe – Ludewa. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Sigrada, kwanza umeuliza maswali mawili, lakini cha msingi swali lako haliendani na swali la msingi. Swali la msingi linataka kujua, kuna utaratibu gani ambao wananchi wanaofanya biashara wafuate pembezoni mwa barabara za *TANROADS*, na majibu yametolewa kuwa wanatakiwa walete maombi, kuna fomu, na *TANROADS* watayashughulikia. Kwa hiyo, nikuombe maswali yako mawili mazuri uyaandike ili yajibiwe. Huyu hana majibu hayo kwa sababu hajajiandaa kujibu kuhusu barabara hiyo ambayo umeisema.

Mheshimiwa Bulaya.

5 FEBRUARI, 2026

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, katika majibu ya swali la nyongeza ambalo Mheshimiwa Waziri amejibu, amejibu kuhusiana na taa za barabarani. Sasa ningependa kujua katika barabara ya kutoka Bunda – Kisolya – Nyamswa, kuna maeneo mengine yana taa, hasa kipande cha *Bunda Store* kwenda Guta mpaka Mwibala. Je, ni lini sasa lile eneo ambalo kuanzia *Bunda Store* kwenda Guta Mwibala litamaliziwa?

SPIKA: Mheshimiwa Bulaya, swali lako haliendani na swali la msingi.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Leo tumeyafupisha maswali kwa sababu tuna uchaguzi, na tuna wagombea 50, na wagombea hawa wakianza kujieleza tutachukua siyo chini ya masaa mawili.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Omari Kipanga familia yake kutoka Kigamboni Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Ndg. Emmanuel Msigwa wa *Media Consultant* kutoka Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Silyvestry Koka ambao ni familia yake kutoka Kibaha Mkoani Pwani. *(Makofi)*

Pia wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, ambao ni wanachama wa Tawi la *CCM Diaspora* nchini Uturuki. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; yupo Ndugu Joseph John - Mkurugenzi wa Gazeti la Kariakoo Leo kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2026

Wapo wanafunzi 38 na walimu watano wa Shule ya Msingi Peace kutoka Jijini Arusha. (Makofi)

Tunao vijana 60 wa Taasisi ya *Capacity Building for Youth Organization* kutoka Jijini Dodoma. (Makofi)

Pia, tunao wanafunzi wa 38 wa Ndaki Insia na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo Kikuu Dodoma. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo wa Spika ulioombwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kuhusu kutojibiwa kikamilifu swali lake la nyongeza katika swali lake la msingi Namba 70.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 2 Februari, 2026 katika Kikao cha Tano cha Mkutano wa Pili wa Bunge la Kumi na Tatu, Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai, aliomba Mwongozo wa Spika kuhusu swali lake la pili la nyongeza katika swali lake la msingi Na. 70. Madai yake ni kuwa, swali hilo halikujibiwa kikamilifu.

Swali la msingi lililoelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa lilikuwa, "Je, lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya Masama, pamoja na nyumba za watumishi wa kituo hicho?"

Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab Seif, Mbunge, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alijibu swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri alikiri kuwa Kituo cha Afya cha Masama, kimejengwa mwaka 1979. Hivyo, miundombinu ya kituo hicho imechakaa na kuwa Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati.

Waheshimiwa Wabuge, Mheshimiwa Mafuwe alipata fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kwa mujibu wa kanuni ya 54 ya Kanuni za Kudumu za bunge 2025. Swali la pili la nyongeza lilitaka kujua, ni lini Serikali itapeleka fedha kujenga *theater* kwa ajili ya upasuaji katika Wilaya ya Hai? Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu swali hilo.

5 FEBRUARI, 2026

Waheshimiwa Wabunge, baada ya majibu ya Naibu Waziri, Mheshimiwa Mafuwe akitumia Kanuni ya 56 ya Kanuni za Bunge, aliomba Mwongozo wa Spika akidai majibu ya Serikali kwa swali lake la pili la nyongeza hayakuridhisha. Kiti kilienda kupitia *Hansard* na kisha kikatoa Mwongozo. Nimepitia *Hansard* na nimejiuliza je, swali la Mheshimiwa Mafuwe, liliendana na swali la msingi?

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 51 inaelekeza kuwa, maswali ya nyongeza ya Waheshimiwa Wabunge yanaweza kuulizwa ili kupata ufafanuzi zaidi kutokana na jibu la swali la msingi. Vilevile kanuni ya 55 (1,2) inaelekeza kuwa swali la nyongeza lisiloendana na swali la msingi, litakataliwa na swali hilo halitaoneshwa kwenye *Hansard*.

Waheshimiwa Wabunge, katika swali lake la msingi, Mheshimiwa Mafuwe alitaka kujua ni lini Serikali itakarabati Kituo cha Afya cha Masama pamoja na nyumba za watumishi? Serikali ilijibu kwamba imetenga fedha na ukarabati wa vituo vya afya ikiwemo Kituo cha Masama. Swali la pili la nyongeza, Mheshimiwa aliuliza ujenzi kuhusu wa *theatre* katika Hospitali ya Wilaya ya Hai. Swali la kuhusu hospitali hiyo haliendani na swali la msingi lililohusu Kituo cha Afya cha Masama.

Waheshimiwa Wabunge, mara kadhaa Mwongozo wa Bunge umekuwa unatolewa kwamba swali la nyongeza linapaswa kuendana na swali la msingi. Maswali ya nyongeza yasiyoendana na swali la msingi yamekuwa yakikataliwa kwa kufutwa kwenye *Hansard*. Mwongozo huu unatokana na masharti ya Kanuni ya 55 (2) ya Banuni za Bunge 2025.

Mwongozo wangu katika ombi la Mheshimiwa Mafuwe ni kuwa, swali lake la pili la nyongeza linakinzana na Kanuni ya 55 (1) kwa kuuliza jambo hilo tofauti na swali lake la msingi. Hivyo, kwa mujibu wa kanuni ya 55 (2) ninaelekeza kufutwa kwenye *Hansard* swali la pili la Mheshimiwa Mafuwe, pamoja na jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri.

5 FEBRUARI, 2026

Ikiwa Mheshimiwa Mafuwe atapenda kupata majibu ya swali lake la nyongeza, anaweza kuleta swali hilo kama swali la msingi. Huo ndiyo Mwongozo wa Spika, umetolewa leo tarehe 5 Februari, 2026.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu uhuru wa majadiliano Bungeni. Wakati wa Bunge likiendelea kujadili hotuba ya Rais, kumetokeza taarifa katika vyombo mbalimbali vya habari, vinavyoeleza kwamba baadhi ya Wabunge wameitwa na *TAKUKURU* ili kuhojiwa kuhusu mchango walioutoa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya Tano ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, nimeona kuwa ipo haja ya kufafanua suala la haki la uhuru wa Majadiliano Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, katika kutekeleza majumu ya Bunge katika kikao cha Bunge, kamati au shughuli nyingine za Kibunge, Wabunge wako huru kutoa mawazo na kufanya majadiliano bila shinikizo, hofu, kuhojiwa, kushitakiwa au kikwazo kingine chochote. Uhuru huo unalindwa chini ya Ibala ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na chini ya Kifungu cha 3(6) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni za Kudumu za Bunge zimeweka wazi masuala yasiyoruhusiwa kujadiliwa Bungeni. Endapo utatokea ukiukwaji, kiti kinaweza kuelekeza kufutwa kwa mchango wa Mbunge usioruhusiwa au kumtaka kufuta mchango wake. Iwapo Mbunge atakaidi maelezo ya kiti, anaweza kupelekwa kwenye Kamati ya Bunge kwa ajili ya uchunguzi.

Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Spika, haijapokea wito wa kumtaka Mbunge, na wala sijatoa kibali kwa Mbunge yeyote kwenda kuhojiwa na *TAKUKURU*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo haya, ninawapongeza Wabunge wote kwa michango yenu yenye tija mnayoitoa kwa manufaa ya Taifa letu. Tuendeleo kutoa michango hiyo kwa kuzingatia Katiba, Sheria na Kanuni za Bunge.

5 FEBRUARI, 2026

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge, kuwa Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, mnamo tarehe 12 Disemba, 2025 alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais, Baraza za Mazingira la Umoja wa Mataifa (*UNEA*).

Kuchaguliwa kwa Mheshimiwa Masauni kushika wadhifa huo ni heshima kubwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na unaakisi dhamira, mchango na msimamo thabiti wa nchi katika kutekeleza sera, mikakati na ahadi za kikanda na za Kimataifa kuhusu ulinzi wa uhifadhi wa mazingira. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linampongeza Mheshimiwa Masauni kwa kuchaguliwa kushika wadhifa huo. (*Makofi*)

Umoja wa Waislamu Bungeni, viongozi wa pendekezo: Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed Mussa Utali; Makamu Mwenyekiti, Amina Good Said; Katibu, Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa; Katibu Msaidizi, Mheshimiwa Asma Ali Mwinyi; na Mweka Hazina, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko na Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda. Taarifa hii imeletwa na Mheshimiwa Mariam Kisangi kwa niaba ya Mheshimiwa Mama Salma Kikwete. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, jana wakati Mheshimiwa Janeth Mahawanga anachangia hotuba ya mipango, alizungumza mambo ya msingi sana, lakini nikamwona Mheshimiwa Waziri Gwajima, kwa utiifu na uzalendo wake akaenda kumfuata Mheshimiwa Mahawanga na kutaka kujua zaidi ili aweze kumsaidia yeye na kusaidia akina mama, wanawake na vijana nchini.

Ninayasema haya kwa sababu nilivutiwa na kitendo cha Waziri kwenda kuuliza kwa Mbunge.

Mheshimiwa Waziri, ninakupongeza sana kwa namna unavyotekeleza majukumu yako kwa utiifu, usahihi na kuhakikisha kuwa azma ya Mheshimiwa Rais na sera zake na mipango yetu inaenda sawasawa na wananchi waridhike kwa kupata majibu sahihi kutoka Serikalini. Hongera sana, Mheshimiwa Waziri. Tutawapongeza

5 FEBRUARI, 2026

Mawaziri na watendaji wote. Pia tutawabana wale wasiofanya majukumu yao. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA, ndc – KATIBU MEZANI:

UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE TAASISI MBALIMBALI

1. Tume ya Utumishi wa Bunge;
2. Wajumbe wa Bunge la Afrika (*PAP*);
3. Jukwaa la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC-PF*);
4. Umoja wa Mabunge Duniani (*IPU*); na
5. Umoja wa Maziwa Makuu (*Great Lakes*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Msimamizi wa Uchaguzi.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE: Waheshimiwa Wabunge, kama inavyoonekana kwenye orodha ya shughuli za Bunge, leo Alhamisi tarehe 5 Februari, 2026 kutakuwa na uchaguzi wa Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge na Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Taasisi mbalimbali za Kibunge.

Waheshimiwa Wabunge, uchaguzi huu unafanyika kwa kuwa nafasi za uwakilishi katika vyombo na taasisi za uwakilishi wa Bunge zimebaki wazi baada ya Bunge la Kumi na Mbili kuvunjwa.

SPIKA: Samahani Katibu.

5 FEBRUARI, 2026

Waheshimiwa Wabunge, si mnasikia wenyewe maneno hayo?

Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba sana tuwe na utulivu wakati Katibu anatoa Miongozo ya Uchaguzi. Uchaguzi huu ni huru na haki, tunataka kila mtu asikilize maelekezo vizuri.

Katibu.

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ninaomba kuendelea.

Waheshimiwa Wabunge, nafasi zilizopo ambazo zinahitaji kujazwa ni hizi zifuatazo: -

1. Tume ya Utumishi wa Bunge;
2. Bunge la Afrika;
3. Jukwaa la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika;
4. Umoja wa Mabunge Duniani; na
5. Jukwaa la Kibunge la Nchi za Maziwa Makuu.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 14 na 15 ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 kwa ujumla wake zinaelekeza kwamba uchaguzi wa Wajumbe wa Tume na Wabunge wanaokwenda katika vyombo vingine ambavyo kwa mujibu wa mikataba na sheria zinazounda vyombo hivyo vinatakiwa viwe na wawakilishi wa Bunge, utafanywa kwa kuzingatia kwa kadiri iwezekanavyo uwiano wa idadi ya Wabunge wa Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni, uwakilishi wa jinsi na pande mbili za Muungano na kwa kuzingatia utaratibu wa Kanuni za Uongozi wa Mabunge hayo iliyoko katika Nyongeza ya Pili na Nyongeza Tano ya Kanuni za Bunge.

5 FEBRUARI, 2026

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia tarehe 27 Januari, 2026 kwamba Wabunge wenye nia ya kugombea nafasi hizo wajaze fomu za maombi na kuzirejesha kabla ya tarehe 3 Februari, 2026 saa 10.00 Jioni, uteuzi umefanyika kwa kuangalia vigezo mbalimbali ambavyo vimejumuisha sifa za kila mgombea aliyejitokeza kuchukua fomu na uwiano wa nafasi.

Hivyo basi, majina yaliyopokelewa na kupendekezwa kwa ajili ya kujaza nafasi hizo pamoja na mgawanyo wa kila nafasi ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Bunge, kwa mujibu wa Kifungu cha 12 (2) cha Sheria ya Uendeshaji wa Bunge, Wajumbe watatu wanaingia kwa mujibu wa nafasi zao ambao ni Spika, ambaye ni Mwenyekiti wa Tume; Naibu Spika, Makamu Mwenyekiti wa Tume; na Waziri anayeshughulikia masuala ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nafasi ambazo zinatakiwa kujazwa kwa njia ya uchaguzi ni saba kwa mujibu wa Kifungu cha 12 (e) cha sheria hiyo. Hivyo basi, Wabunge waliochukua fomu na kurejesha ili kujaza nafasi hizo ni 14 na walioteuliwa ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kundi A ni Wabunge kutoka Chama Tawala, nafasi tano, kwa mgawanyo ufuatao:-

Tanzania Bara wanaume walioteuliwa ni wanne na wanaotakiwa ni wawili kati ya wafuatao: -

1. Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (CCM);
2. Mheshimiwa Dkt. William Charles Mahera (CCM);
3. Mheshimiwa Patali Shida Patali (CCM); na
4. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere (CCM).

Mheshimiwa Spika, kundi B, Tanzania Bara wanawake walioteuliwa ni wawili na anayetakiwa ni mmoja kati ya wafuatao: -

5 FEBRUARI, 2026

1. Mheshimiwa Dkt. Catherine Canute Joachim (CCM); na
2. Mheshimiwa Asha Salum Motto (CCM).

Mheshimiwa Spika, kundi C, Zanzibar wanaume walioteliwa ni wawili na anayetakiwa ni mmoja kati ya wafuatao: -

1. Mheshimiwa Haji Amour Haji (CCM);
2. Mheshimiwa Amjadi Ussi Salum Pondeza (CCM).

Mheshimiwa Spika, kundi D, Zanzibar wanawake walioteuliwa ni wawili na anayetakiwa ni mmoja kati ya wafuatao: -

1. Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma (CCM); na
2. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud (CCM).

Mheshimiwa Spika, kundi B ni wa Wabunge wa Kambi ya walio Wachache Bungeni walioteuliwa ni wawili na wanaotakiwa ni wawili. Hawa watapigiwa kura ya “Ndiyo” au “Hapana”: -

1. Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza (CHAUMMA); na
2. Mheshimiwa Ado Shaibu Ado (ACT-Wazalendo).

Mheshimiwa Spika, kundi B, Wajumbe wa Bunge la Afrika (PAP) nafasi zilizopo ni tano. Wabunge waliochukua na kurudisha fomu ni 17 na walioteuliwa ni kama wafuatao: Kundi A, Wabunge wanawake walioteuliwa ni wawili na anayetakiwa ni mmoja.

1. Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha; na
2. Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule.

Mheshimiwa Spika, kundi B, Wabunge wa Zanzibar walioteuliwa ni wawili anayetakiwa ni mmoja.

5 FEBRUARI, 2026

1. Mheshimiwa Imamu Mtumwa Vuai; na
2. Mheshimiwa Seleman Mohamed Rashid.

Mheshimiwa Spika, kundi C, Wabunge wa Tanzania Bara walioteuliwa ni wanne na wanaotakiwa ni wawili kati ya wafuatao:-

1. Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula;
2. Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari;
3. Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima; na
4. Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo.

Mheshimiwa Spika, kundi B, Wabunge Kambi ya walio Wachache Bungeni nafasi ni moja. Aliyejitokeza ni mmoja Mheshimiwa Rashid Habib Ali (ACT-Wazalendo), huyu atapigiwa kura ya "Ndiyo" au "Hapana".

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu ni Wajumbe Jukwaa la Mabunge ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC-PF). Nafasi zilizopo ni tano, ambapo kwa mujibu wa Katiba ya SADC nafasi moja kundi A hujazwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Mabunge ya Wanawake ambaye ni Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako. Hivyo Wabunge waliochukua na kurudisha fomu kwa nafasi nne zilizobaki ni 16 na walioteuliwa ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kundi B, Wabunge wa Zanzibar walioteuliwa ni wawili na anayetakiwa ni mmoja.

1. Mheshimiwa Kassim Hassan Haji; na
2. Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya.

Mheshimiwa Spika, kundi C, Wabunge wa Tanzania Bara walioteuliwa ni wanne na wanaotakiwa ni wawili kati ya wafuatao: -

5 FEBRUARI, 2026

1. Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba;
2. Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda;
3. Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela; na
4. Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma.

Mheshimiwa Spika, kundi B, Wabunge wa Kambi ya Walio Wachache Bungeni, nafasi ni moja, na aliyejitokeza ni mmoja. Mheshimiwa Mohamed Khalfan Issa wa ACT-Wazalendo na huyu atapigiwa kura ya "Ndiyo" au "Hapana".

Mheshimiwa Spika, kundi la nne ni Wajumbe wa Umoja wa Mabunge Duniani (*IPU*). Nafasi zilizopo ni saba na Wabunge waliochukua na kurudisha fomu ni 22 na walioteuliwa ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kundi A, Wabunge wanawake walioteuliwa ni wawili. Anayetakiwa ni mmoja kati ya wafuatao: -

1. Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana; na
2. Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge.

Mheshimiwa Spika, kundi B, Wabunge wa Zanzibar walioteuliwa ni wawili na anayetakiwa ni mmoja.

1. Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid; na
2. Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar.

Mheshimiwa Spika, kundi C, Wabunge wa Tanzania Bara, walioteuliwa ni nane na wanaotakiwa ni wanne.

1. Mheshimiwa *Engineer* Fatma Ally Rembo;
2. Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu;

5 FEBRUARI, 2026

3. Mheshimiwa Asha Juma Feruz;
4. Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi;
5. Mheshimiwa Emmanuel John Kambay;
6. Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Qambaji Nuwas;
7. Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda; na
8. Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume.

Mheshimiwa Spika, kundi D, Wabunge wa Kambi ya Walio Wachache Bungeni nafasi ni moja, na aliyejitokeza ni mmoja Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye ACT-Wazalendo na huyu atapigiwa kura ya “Ndiyo” au “Hapana”.

Mheshimiwa Spika, kundi la mwisho ambalo ni Kundi namba tano ni Wajumbe wa Jukwaa la Kibunge la Nchi za Maziwa Makuu. Nafasi zilizopo ni tano na Wabunge waliochukua na kurudisha fomu ni 14 na walioteuliwa ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kundi A, Wabunge Wanawake walioteuliwa ni wawili, anayetakiwa ni mmoja.

1. Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula; na
2. Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel.

Mheshimiwa Spika, kundi B, Wabunge wa Zanzibar walioteuliwa ni wawili anayetakiwa ni mmoja.

1. Mheshimiwa Saidi Salim Hamad; na
2. Mheshimiwa Sadifa Juma Khamisi.

Mheshimiwa Spika, kundi C, Wabunge wa Tanzania Bara walioteuliwa ni wanne. Wanaotakiwa ni wawili kati ya wafuatao: -

5 FEBRUARI, 2026

1. Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa;
2. Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala;
3. Mheshimiwa Festo Richard Sanga; na
4. Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

Mheshimiwa Spika, kundi B, Wabunge wa Kambi ya Walio Wachache Bungeni, nafasi ni moja. Aliyejitokeza ni mmoja ambaye ni Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo wa ACT-Wazalendo. Huyu naye atapigiwa kura ya "Ndiyo" au "Hapana".

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo yangu hayo ya msingi kwa kila nafasi, utaratibu wa kupiga kura utakuwa ni ule ule wa kikanuni ambapo Spika atawaita Wabunge wajieleze kwa wapigakura na kutakuwa na fursa ya kuuliza maswali matatu kama yatakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, wakati wa kujieleza kwa wagombea wa nafasi ya Tume ya Utumishi wa Bunge, kila Mgombea anaweza kujieleza kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza bila kuchanganya lugha. Aidha, kwa wagombea wa nafasi za vyombo vingine wa uwakilishi, kila mgombea atatakiwa kujieleza kwa Lugha ya Kiingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katibu atapata idadi ya kura na masanduku ya kura yataletwa hapa mbele ya Bunge. Kila Mbunge atapewa karatasi ya kura kwa kundi moja na baada ya kupiga kura kwa kundi hilo kura zitakusanywa kabla ya kuendelea na makundi yanayofuata.

Mheshimiwa Spika, karatasi ya kura itakuwa na maelekezo kuhusu namna ya kupiga kura katika kila kundi la uchaguzi.

Baada ya kumaliza kupiga kura, kura zitahesabiwa chini ya Katibu wa Bunge na Wawakilishi watano watakaoteuliwa na Spika.

Baada ya kukamilisha zoezi la kuhesabu kura, Katibu atatangaza matokeo ya kura, na mwisho Spika atahitimisha kwa kutoa pongezi kwa washindi kwa kadiri atakavyoona inafaa.

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, sasa ninaomba zoezi letu la uchaguzi lianze. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Katibu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa ratiba yetu tunaanza na Tume ya Utumishi wa Bunge. Ninaanza kumwita Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, lakini tumeambiwa ana dharura. Mgombea wa pili ni Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera Charles utakaa hapo hapo ulipo na kuomba kura.

MHE. DKT. WILSON C. MAHERA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaitwa Wilson Mahera Charles, nimeomba nafasi ya Ujumbe wa Utumishi wa Bunge. Mimi nina elimu ya *Ph.D* upande wa hesabu, lakini nimewahi kuwa Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ambapo nimekuwa nikisimamia watumishi zaidi ya 3,000. Pia, baada ya hapo nikawa Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambapo nilisimamia masuala ya uchaguzi wa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, baadaye nikateuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambapo nilihudumu kwa muda wa mwaka mmoja na nusu. Baada ya hapo nikateuliwa kwenda Wizara ya Elimu kama Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu ambapo nilihudumu. Sasa mimi ni Mbunge kutoka Jimbo la Butiama.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kura zenu ili niweze kuwa Kamishna wa Tume hii ya Utumishi wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Maswali.

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, hatuna.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Patali Shida Patali.

5 FEBRUARI, 2026

MHE. PATALI S. PATALI: Mheshimiwa Spika, kama ulivyonitambulisha, nirudie, ninaitwa Patali Shida Patali.

Mheshimiwa Spika, nimeomba nafasi ya Ujumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge. Nimeomba nafasi hii kwa sababu mbili: Kwanza, mpaka ninaingia kwenye Bunge hili nimekuwa nikihudumu kama Afisa Utumishi kwa miaka yangu takribani 15.

Mheshimiwa Spika, ninatambua Tume hii majukumu yake makubwa ni kusimamia ajira, maslahi, miundo pamoja na sera za watumishi. Tume hii inaidhinisha bajeti za watumishi na ninyi Wabunge wote mliopo katika Bunge hili, ili kufanya majukumu yenu sawia na katika akili ya msawazo, mnahitaji watumishi wanaoweza kuwahudumia wakiwa katika hali ambayo ni tulivu na hawana *stress*.

Mheshimiwa Spika, niliyepo hapa mbele yako na Wabunge wote wa Bunge hili Tukufu mara ya mwisho nimehudumu kama Mkurugenzi wa Utumishi na Utawala, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Mbeya chini ya Wizara ya Maji. Nimefanya kazi vizuri, ninafahamu namna bora ya kuwafanya watumishi wafanye kazi yao vizuri ikiwa ni pamoja na kuwahudumia Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninafahamu moja ya jukumu kubwa la Bunge hili Tukufu ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Vilevile, kazi kubwa ya Bunge hili iliyojificha ni kutengeneza na kuandaa viongozi wa kesho. Ninafahamu kabisa mna nafasi kubwa ya sisi viongozi tulioingia katika Bunge hili kutuandaa na kutufinyanga ili tuwe bora kwa ajili ya kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nipo mbele yenu kuomba kura kwa heshima kubwa, mnipe kura za "Ndiyo" nipate kuwa Mbunge ambaye ninawakilisha Tume hii ya Utumishi wa Umma hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana, ninaomba kura zenu.

SPIKA: Maswali.

5 FEBRUARI, 2026

WABUNGE: Mheshimiwa Spika, hakuna.

SPIKA: Mheshimiwa Getere. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge! *(Makofi/Kicheko)*

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, kwa jina ninaitwa Boniphace Mwita Getere...

SPIKA: Mheshimiwa Getere, subiri kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, tuna kanuni za uchaguzi. Msiwe mnamchuuza mtu, mkawa mnampa imani kumbe mnamcheza shere hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa tumwache ajieleze, halafu mtafanya maamuzi ninyi wenyewe. Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, kwa jina ninaitwa Boniphace Mwita, maarufu kama mzee wa taarifa fupi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hawa Wabunge wote tunafahamiana na wengi wanafahamu uwezo wangu wa kuwatetea. Kwa heshima na taadhima ninaomba kura zenu, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Catherine Joachim.

MHE. CATHERINE C. JOACHIM: Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, niliyesimama mbele yenu ninaitwa Catherine Canute Joachim. Nimesimama hapa kuomba kura zenu kama Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kwamba kazi yetu sisi Wabunge ni kutunga sheria, lakini ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa weledi, haki na maarifa, sisi kama Wabunge tunahitaji kuwa na maslahi yanayotufanya tutekeleze majukumu yetu kwa makini. Siyo sisi tu, hata watumishi mbalimbali ambao wanatuhudumia.

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, ninaahidi kwamba mkinichagua nitawatumikia kwa uaminifu mkubwa, weledi na usiri. Ninaomba kura zenu ili niweze kuwatumikia Ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Asha Salum Motto.

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaitwa Asha Salum Motto, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mtwara.

Waheshimiwa Wabunge wote, kwa heshima na taadhima ninaomba kura zenu kwa nafasi hii ya kuwa mwakilishi wenu Tume ya Utumishi wa Bunge. Nipo tayari kuwatumikia kwa uwezo wangu wote, kuwatetea na kuwasimamia maslahi yenu kwa nafasi hiyo mtakayonipa hivi punde.

Waheshimiwa Wabunge nina uzoefu siyo sana, lakini nina imani nitamudu na kutekeleza yale yote ambayo tutayajadili kwa pamoja. Kabla ya kufika hapa Bungeni nimeshashika nafasi mbalimbali katika utumishi. Nimekuwa Katibu wa Wanawake Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania, nimekuwa Mwenyekiti wa Wanawake Chama cha Wafanyakazi TUGHE, Mkoa wa Mtwara, nimekuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la UWT Taifa.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa nafasi hiyo tu, ninao uwezo mkubwa sana wa kusimama na ninyi na kutetea maslahi yenu. Kamwe sitakuwa na uoga, naomba mnamini, naomba kura zenu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Maswali, maswali, maswali.

WABUNGE FULANI: Hakuna.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwenye nafasi hizi za Tume za upande wa Bara wanaume mtachagua, mtapiga kura mbili tu na kwa upande wa wanawake Bara mtachagua kura moja tu. Tutaanzia na Zanzibar wanaume, na hapa vilevile wapo wagombea wawili,

5 FEBRUARI, 2026

lakini mtapiga kura moja. Imeandikwa katika karatasi. Kwa hiyo, wala msipate taabu. Sasa namwita Mheshimiwa Haji Amour Haji.

MHE. HAJI AMOUR HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa jina ninaitwa Haji Amour Haji, ni Mbunge wa Jimbo la Pangawe Zanzibar. Nimesimama mbele yenu Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kuomba nafasi ya Utumishi wa Bunge, ambayo kwa kifupi tunasema kwamba ni nafasi ya Ukamishna ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nami niliyesimama mbele yako ninayeomba nafasi hii, ninaomba nikiwa kama nina nafasi au nina uteule wa kuwa kama Daktari katika masuala ya uongozi pamoja na masuala ya utu. Vilevile ni Balozi wa Amani ambaye tayari nimepatiwa nafasi hiyo kama ni *Universal Peace Federation*. Hata hivyo, pia katika masuala ya kiutendaji, kwa upande wa Zanzibar nimewahi kuhudumu katika nafasi ya Bodi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa kipindi cha miaka sita.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo nimefanya kazi mbalimbali ambazo ni za ndani ya Serikali na ndani ya binafsi.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, niliyesimama mbele yenu hapa, naomba nafasi hii ili kuweza kuwatumikia kwa dhati ya moyo wangu nikiwa kama mtumishi wenu katika nafasi ya Utumishi wa Bunge kwa nafasi ya Ukamishna. Natumai kwamba nimeomba kwa sababu ninaweza na nimewahi kuhudumu kwa Wabunge wa Zanzibar kama ni Mwenyekiti wa Wabunge kwa kipindi cha miaka mitano.

Naomba kura zenu Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

SPIKA: Maswali, maswali, maswali. Mheshimiwa Amjadi Ussi Salum Pondeza. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Hakuna, hakuna.

MHE. AMJADI USSI SALUM PONDEZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuomba kura. Mimi naitwa

5 FEBRUARI, 2026

Amjadi Ussi Salum Pondeza, ni Mbunge kutokea Zanzibar, Jimbo la Chumbuni na niko hapa kwa kipindi zaidi ya viwili na hiki ni cha tatu. Nina uzoefu wa uongozi kuanzia kwenye chama changu na kwenye taasisi za binafsi ambazo nimekuwa nikiziongoza zaidi ya taasisi sita ziko chini yangu.

Mheshimiwa Spika, nimewiwa nisimame hapa nigombe nafasi hii kwa ajili ya kuwawakilisha Wabunge wenzangu na kwa ajili ya kutetea maslahi yao. Uzoefu wangu, Wabunge wengi mnanielewa, nikianza kusema tutachukua muda kama ulivyosema Mheshimiwa Spika. Naomba kura zenu Wabunge wote. *(Makofi)*

SPIKA: Kundi hili, wanaume wawili kutoka Zanzibar, nafasi ni moja tu. Sasa tunalo kundi la Zanzibar wanawake, wako wagombea wawili: Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Mheshimiwa Mgeni.

MHE. MGENI HASSAN JUMA: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Waheshimiwa Wabunge, ninaitwa Mgeni Hassan Juma, ni Mbunge kutokea Viti Maalum vya NGO's. Vilevile ninatoka Mkoa wa Mjini.

Waheshimiwa Wabunge, nimesimama hapa kuomba kura zenu za "Ndiyo" kwa nafasi ya Ukamishna ya Tume ya Utumishi. Vilevile kwa heshima kubwa sana, naomba mnipe fursa hii, na kwa sababu nina uzoefu mkubwa sana katika kipindi changu chote cha kuwa mwanasiasa nimeanza kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nimekuwa Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi kule Zanzibar, nimekuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wawakilishi Wanawake kule Zanzibar kwa kipindi cha miaka 10.

Mheshimiwa Spika, katika nafasi zangu zote hizo nimezitumikia vizuri sana; nimekuwa nikishirikiana na wenzangu na hapa kuna Wabunge wengi ambao tulikuwa tunafanya kazi pamoja.

5 FEBRUARI, 2026

Kwa hiyo, ndugu zangu Wabunge, kwa heshima kubwa sana naombeni mnipe kura za “Ndiyo” kwa sababu uwezo ninao, nia ninayo na maarifa vilevile ninayo ya kufanya kazi katika Tume hii ili niweze kusaidiana na uongozi wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuomba wewe binafsi kura yako, pia nawaomba Mawaziri wote kura zao. Pia nawaombeni ninyi Wabunge wenzangu ambao tutafanya kazi pamoja kwa kushirikiana ili kuhakikisha kwamba Bunge letu linakwenda vizuri. Nashukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Khadija Aboud.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Niliyesimama mbele yenu, naitwa Khadija Hassan Aboud, ni Mbunge, kwa sasa naingia kipindi cha tatu. Nimekuwa Mbunge kutokea mwaka 2015. Waheshimiwa Wajumbe katika utumishi wangu wa Chama na Serikali niliwahi kuwa Mkurugenzi wa Tamasha Mila na Sanaa kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Mstaafu. Nilikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu kuanzia mwaka 2012 - 2017 pale ambapo lilivyotoka agizo la chama. Aidha, uchague kwenye chama au kwenye mambo mengine. Kwa hiyo, tayari kipindi hicho nilishakuwa Mbunge nikaachia kule. Nimekuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa kwa vipindi vitatu mfululizo kuanzia mwaka 2002 - 2017. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe katika kazi zangu ndani ya Chama na Jumuiya, pia nimewahi kuwa Katibu wa Vijana wa Mkoa wa Mjini Unguja, nimewahi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Vijana Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nimewahi kuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Vijana Taifa kwa vipindi vitatu mfululizo. Nimeshakuwa Katibu Msaidizi wa Chama cha Mapinduzi Ofisi Kuu ya CCM Zanzibar, Idara ya Itikadi na Uenezi. Katika historia yangu ya kisiasa wakati niko natumikia nafasi ya Ukurugenzi kule Zanzibar, toleo la Serikali likaja

5 FEBRUARI, 2026

nikaambiwa, kwa sababu wewe ni Mkurugenzi na huku ni mwanasiasa, uchague moja; siasa au kazi. Waheshimiwa Wajumbe nikauacha Ukurugenzi, nikabaki na Ujumbe wa NEC.

Waheshimiwa Wajumbe kwa kumalizia, ... *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Aboud omba kura.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, uwezo wa kuwatumikia ninao, shida za Wabunge nazijua, matatizo ya Wabunge nayafahamu vizuri, naomba kura zenu, naomba kuwatumikia. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Maswali, maswali, maswali.

WABUNGE FULANI: Hakuna, hakuna.

SPIKA: Waheshimiwa tunakwenda kundi la Wabunge walio wachache Bungeni, wako wawili, na hapa ni kupiga kura ya "Ndiyo" au "Hapana". Wako wawili, mnapiga "Ndiyo" au "Hapana." Mheshimiwa Agnesta Kaiza, ana dharura. Mheshimiwa Ado Shaibu Ado.

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Spika, ninaitwa Ado Shaibu Ado, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini. Kwa heshima ninasimama mbele ya Bunge hili kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wanichague kuwa Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, ahadi yangu ni moja tu, nitatetea kwa vitendo maslahi ya Bunge hili, maslahi ya Wabunge na maslahi ya Watumishi wa Bunge ambayo kwa hakika ndiyo mamlaka ya Tume ya Utumishi wa Bunge. Kwa unyenyekevu mkubwa ninaomba kura zenu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Maswali, maswali, maswali.

WABUNGE FULANI: Hakuna, hakuna.

5 FEBRUARI, 2026

SPIKA: Ahsanteni, Waheshimiwa sasa tunakwenda kundi la PAP. Wagombea Tanzania Bara kundi A Wabunge wanawake. Nafasi ni moja wako wawili. Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha.

HON. LULU G. MWACHA: Honourable Speaker, Honourable Members of Parliament, good morning. My name is Lulu Mwacha, Member of Parliament, representing the youth of our beloved country. I hold a Master's Degree of Arts in Peace and Security, also a Bachelor's of International Relations and Diplomacy. (Applause)

Honourable Speaker, I stand before you kindly requesting for your votes, your support and also your trust to believe in me so that I can be your representative in the Pan-African Parliament. (Applause)

Honourable Speaker, I dedicate myself to go and promote peace and security, and also to fostering our foreign policy which is economic diplomacy. I will also work to strengthen our relationship with other African Nations. Furthermore, I will ensure that the Tanzanian voice is heard in the international arena and in regional integration, while promoting economic development and also welfare of our people. (Applause)

Honourable Speaker, lastly, I will make sure I carry our flag with respect, dignity, and integrity.

Thank you so much. Once again, I kindly request your votes. Thank you very much, Honourable Members of Parliament. (Applause)

SPEAKER: Honourable Dr. Neema Peter Majule.

HON. DR. NEEMA P. MAJULE: Honourable Speaker, and Honourable Member of Parliament, Distinguished Guests and Distinguished Leaders, Ladies and Gentleman. My name is Neema Peter Majule. I am a member of Parliament under special seats but also, I am regional women wing leader for Dodoma, but also I am in charge of all women wing leaders of the whole country.

5 FEBRUARI, 2026

Honourable Speaker, not only that, I have experience in working in politics being a regional women's wing leader, I have served the community for more than 10 years. So, I know how to work from grass root level, mobilizing women, mobilizing resources to start income-generating activities for them. (Applause)

Honourable Speaker, in addition, not only that, I was HIV/AIDS coordinator for almost 10 years where I was able to travel over the whole region of Africa and overseas. (Applause)

Honourable Speaker, I travel to Brazil, USA, UK and also in my continent. I was able to travel to South Africa, Zambia, Uganda and Kenya to represent my country on HIV/AIDS, as I served as the Coordinator for HIV/AIDS over the whole country. Through these experiences, I gained valuable exposure and strengthened my public speaking skills. (Applause)

Honourable Speaker, moreover, I realize that African country we share the same challenges such as health problem; all of us we face tropical diseases such as epidemic and pandemic, and also communicable and non-communicable diseases. Being in a continent, I will help other leader to solve this problem including social and economic problems.

Please Members of Parliament and Honourable Speaker give me this chance, I will represent women in Pan African Parliament, thank you. (Applause)

SPEAKER: Thank you very much honourable. Now we shift to Members of Parliament Zanzibar. We have two candidates, we have to choose one. The first candidate is Imamu Mtumwa Vuai.

HON. IMAMU MTUMWA VUAI: Honourable Speaker, Honourable Member of Parliament in front of you my name is Imamu Mtumwa Vuai, a Member of Parliament from Magomeni Zanzibar. I contest for Member of Pan-African Parliament. I pursue Postgraduate Diploma in Economic Diplomacy and Bachelor's Degree of Conflict Resolution and Peace Building which fits the position.

5 FEBRUARI, 2026

As Africa proverb say "If you want to go fast, go alone, if you want go far go together". I humbly ask your support and yes votes, so that we may go together in serving Tanzania and Africa.

Thank you, honourable members, thank you Honorable Speaker for your time and attention. (Applause)

SPEAKER: Any questions, any questions. Labda niseme Kiswahili. Maswali, maswali.

WABUNGE: Hakuna.

SPEAKER: Honourable Suleiman Mohamed Rashid.

HON. SULEIMAN MOHAMED RASHID: Honourable Speaker, thank you. My fellow Member of Parliament, my name is Suleiman Mohamed Rashid, a Member of Parliament from Mwera Constituency Zanzibar.

I worked in the revolution government of Zanzibar, different position and different institution. I worked as a Planning and Static Officer from Zanzibar Electricity Corporation. I also served as the Acting Director of the Urban Municipal Council for nine months. Furthermore, I was the Director of Administration and Personnel from the President Office, Finance and Planning. (Applause)

Honourable Speaker and Honourable Member of Parliament I hold a Bachelor's Degree in Economics from Zanzibar University. I also obtained a Postgraduate Diploma in Leadership from Uongozi Institute, and I have a Master's Degree in Monitoring Evaluation from The Open University of Tanzania. I have attended different seminar and workshop in and outside of Tanzania such as China. I am experienced and exposed, that I am ready to fit in this position. (Applause)

Honourable Speaker, I am very interested in this position because I want to influence four things: - (Applause)

- (i) Advance economic integration and trade;
- (ii) Influence continental policy;

5 FEBRUARI, 2026

- (iii) Promoting regional stability and governance; and*
- (iv) Direct benefits for Tanzania citizens.*

Honourable Speaker, and my fellow Members of Parliament, please vote for me. My name is Suleiman Mohamed Rashid from Zanzibar. Ahsanteni (Applause)

SPEAKER: *Members, any questions? Thank you very much Honourable.*

Now we go to group C which is Mainland. Member of Parliament from Mainland we have two position and we have four candidates. The first one is Honourable Mariam Anzuruni Mungula. (Applause)

HON. MARIAM A. MUNGULA: *Honourable Speaker, thank you.*

Honourable Speaker and Distinguished Members of Parliament, standing before you my name is Honourable Mariam Anzuruni Mungula and I am vying for the position of Pan-African Member of Parliament Representative.

Honourable Speaker, I am an Advocate of the High Court of Tanzania and I held over 20 years of working experience in various positions including leadership positions which required me to have negotiating and leadership skills as well. (Applause)

Honourable Speaker, I am deeply committed to our country's principles of unity, peace and development which have always been at the hearts of our foundation as a nation. If given this opportunity to represent our country in the Pan-African Parliament, I will ensure to work hard and tirelessly in order to make sure that these principles and any other interest that we might have as a country are guarded, protected, defended as well as negotiated within the organ and our continent at large. (Applause)

Honourable Speaker and Distinguished Members of Parliament, I humbly ask for your votes, thank you. (Applause)

5 FEBRUARI, 2026

SPEAKER: *Members, any questions? Honourable Matiko.*

HON. ESTHER N. MATIKO: *Honourable Speaker, thank you. I just wanted to know, if we elect Honourable Mariam today, how will she balance the national interest vis a vis the continental goals?*

HON. MARIAM A. MUNGULA: *Thank you Distinguished Member, as have I already stated, I will always ensure that our nation's interest comes first before anything else. (Applause)*

SPEAKER: *Thank you very much. Honourable Joshua Samwel Nassari.*

HON. JOSHUA S. NASSARI: *Honourable Speaker, thank you. Honourable Members of this August House, my name is Joshua Nassari, I bring with me experience from having worked as a Member of Parliament in this House. At the same time, I was honoured also to be appointed by the Head of the State, Honourable Dr. Samia Suluhu Hassan to serve as the District Commissioner for several districts in this country. (Applause)*

Honourable Speaker, first, I served in Bunda District (Mara Region), then I moved to Singida Region (Iramba District) which is basically our Prime Minister's Constituency and I served there with honour. I was later transferred to Monduli District in Arusha Region and then, Magu District in Mwanza. (Applause)

Honourable Speaker, my education brings a huge value with me as I received my Bachelor's Degree at the University of Dar es Salaam with Honors. One of my teachers or one of my professors being Dr. Bashiru Ally who is here today as a Minister. In 2016, I completed and managed to win a scholarship with Chevening which is Official British Governed Sponsored Programs and I received a Master's Degree in International Relations and Democratic Politics at the University of Westminster in Central London UK and then in 2020, I also graduated with another Master's Degree in International Development and Policy from the University of Chicago at the School of Public Policy which was basically sponsored by the Obama Foundation. (Applause)

5 FEBRUARI, 2026

Honourable Speaker, it was a special program that was crafted by University of Chicago at the School of Public Policy and the Obama Foundation to enhance the global identified young change makers ...

SPEAKER: *Honourable Nassari, could please solicit for your vote.*

HON. JOSHUA S. NASSARI: *Honourable Speaker, sorry?*

SPEAKER: *Could please solicit for your vote?*

HON. JOSHUA S. NASSARI: *Honourable Speaker and Honourable Members, I humbly come before you to ask for your vote so that I can fly our flag high in the Pan-African Parliament famously known as Bunge la Afrika. I want to assure you that by having in there (in the House) you guys will not make a mistake and you will have a right representative. Kwa hiyo, ninaombeni kura zenu. (Applause)*

Honourable Speaker and Honourable Members, thank you. (Applause)

SPEAKER: *Any questions, any questions? Honourable Thomas Mgonto Kitima, could you please address the Members?*

HON. THOMAS M. KITIMA: *Honourable Speaker, Ministers, and all Members of Parliament, Kazi na Utu.*

MEMBERS OF PARLIAMENT: *Tunasonga Mbele.*

HON. THOMAS M. KITIMA: *Honourable Speaker, my name is Thomas Mgonto Kitima, I am standing before you this morning as the candidate of Pan-African Parliament. I am the holder of a Master's Degree of Revenue Law and the Administration from the University of Dar es Salaam, and a Postgraduate Diploma in International Economy Diplomacy from the College of Foreign Relations there at Kurasini, Dar es Salaam.*

Honourable Speaker, I am committed to present all matters which are missions of this country and this Parliament to the Parliament

5 FEBRUARI, 2026

which I am contesting for. The Parliament of Africa, or Pan-African Parliament is the platform whereby African people and the organizations from their grassroots come together, discuss their matters, and make decisions for the issues which are challenging them, and which are problem to the whole continent.

Honourable Speaker, this is the organ under the protocol which ensures this continent remains in peace. So, by saying that, I am the right person because I am well experienced from attending various international forums like SACCA Congress which held in the various countries like Kenya, Uganda, and Rwanda. Also, I am an energetic person, honest person, and well prepared to represent my country by portraying good image as Mwalimu Nyerere did at his era and what Mama Samia is doing at this time. (Applause)

Honourable Speaker, I am humbly requesting you to vote for Thomas Mgonto Kitima as representative of this Parliament. Thank you. (Applause)

SPEAKER: Any questions from the members? Honourable Dr. Selemani Said Jafo.

HON. DR. SELEMANI S. JAFO: Honourable Speaker, Mussa Azan Zungu; I would like to recognize the presence of Honourable Daniel Baran Sillo, the Deputy Speaker of this National Assembly; Honourable Ministers and Deputy Ministers present; Honourable Members of Parliament; Mr. Baraka Leonard Clerk of National Assembly, the one prepared this whole logistics that has been going on; Ladies and gentlemen; Good morning.

MEMBERS OF PARLIAMENT: Good morning.

HON. DR. SELEMANI S. JAFO: Honourable Speaker, first of all, I would like to take this opportunity to thank the Almighty God for granting me this opportunity to stand at this podium. And also, I would like to extend my sincere gratitude to Her Excellency Dr. Samia Suluhu Hassan, the President of the United Republic of Tanzania, and the

5 FEBRUARI, 2026

Chairperson of Chama cha Mapinduzi, a champion of diplomacy and development in the Africa. (Applause)

Honourable Speaker, I would like also to extend my heartfelt gratitude to the member of the Central Committee, for nominating me to stand here as a candidate for Pan-African Parliament. (Applause)

Honourable Speaker, shortly I would like maybe to brief about my background experience. One, as you all know that, I was a former Minister for Industries and Trade, responsible for negotiation on trade matters, national and international trade. But also, I was a former Minister for Environment and Union Matters in the Vice President's Office responsible for all Union matters, as I think you all know we addressed almost 14 challenges that were facing our union. But also, I was a former Minister for Regional and Local Government Authorities for almost four years. I was also, the chairperson of the African Continental Free Trade Area for one year, serving the African Continent on all issue related to the business. (Applause)

Honourable Speaker, also, I was a Member of SADC Parliamentary Forum for the period 2012 to 2015. In that experience, I was elected to be a treasurer for SADC Parliamentary Forum with the outstanding performance on financial matters. I was the one innovated a new system for finance monitoring in the SADC Region and system called the JAFO Financial Communication Protocol. That is a successful story that I have. (Applause)

Honourable Speaker, from this bulk of boldness of experience, I believe that Members of Parliament will select me and I am sure that I will be the one who support all the government issues. I will be the one who represent the government matters, to share success stories because as you know that the African Parliament is a platform that we have to exchange the idea and share success stories. (Applause)

Honourable Speaker, we Tanzanians, we have to tell our African people, that we are on the path of Africa we want. We have a project called Inga – Dam but Tanzania, we showed the success story by

5 FEBRUARI, 2026

having Nyerere Hydro Dam. This is a successful story, and we have to share this success story.

Apart from that, among the flagship projects, which were supposed to be implemented and the Africa agenda we want, is that to have connection of SGR. Unfortunately, many countries failed, except Tanzania. So, these are success stories that we have to share in the Pan-African Parliament.

Honourable Speaker, my humble request to the Members of Parliament, please, I need your support. I need your vote. I need your endorsement. (Applause)

Honourable Speaker, I thank you. (Applause)

SPEAKER: Thank you very much, now we have one position from the Members of Parliament from the minority group, one candidate and one position, Honourable Rashid Habib Ali.

HON. RASHID HABIB ALI: Honourable Speaker and Honourable Members, ladies and gentlemen, my name is Rashid Habib Ali, a current Member of Tanzania Parliament, and I am a Master's holder of Public Administration and Human Resource Management in Zanzibar University, and I am a degree holder of International Relations and Diplomacy also from Zanzibar University. I am here to ask you for your vote and your support to represent you in Pan-African Parliament with understanding that Tanzania interest is first than all.

Honourable Speaker, thank you. Vote for Rashid Habib Ali. (Applause)

SPEAKER: Any questions? Hakuna, ahsanteni.

Now we have Members of the SADC PF. We will start with Honourable Kassim Hassan Haji from Zanzibar. Position is one and we have two candidates.

5 FEBRUARI, 2026

HON. KASSIM HASSAN ALI: Honourable Speaker, Honourable Members of Parliament, I seek your vote to represent Tanzania at SADC Parliamentary Forum with proven experience from my previous service. I am ready to advance our nation and the Parliamentarian interests. I respectfully request your support. Thank you. (Applause)

SPEAKER: Thank you very much. Any questions? Thank you very much. Now we have another candidate, Honourable Ali Haidar Madeweyya please address the members.

HON. ALI HAIDAR MADEWEYYA: Honourable Speaker and my fellow Members of Parliament, my name is Ali Haidar Madeweyya, I have a Bachelor degree of Supply Chain Management, I know the big role of SADC for Tanzanians. I know there are some member states that are land locked. I will try to push some member states to use Dar es Salaam Port for the development of our country (Tanzania). (Applause)

Honourable Speaker, and other Members of Parliament, once again, vote for Madeweyya. Thank you. (Applause)

SPEAKER: Any questions? Thank you very much. Now we go to the Mainland. We have four candidates and we have only two positions.

We start with Honourable Lutengano George Mwalwiba.

HON. LUTENGANO G. MWALWIBA: Honourable Mr. Speaker, Honourable Ministers, My colleagues Member of Parliament in this House. My name is Lutengano George Mwalwiba, a Member of Parliament from Busokelo in Mbeya Region. I am one among those who are just contesting the post of being a Representative in SADC Parliamentary Forum.

My colleagues, I know that we all understand involvement of our country in political freedom liberation of these member states of the SADC. Right now, we have only one common goal for all member states, to ensure that we achieve economic liberation together.

5 FEBRUARI, 2026

Honourable Speaker, our country has got a very good policy and our foreign policy is standing for the for diplomatic economy. What is to be done in that place is to ensure that the interests of our country is well safeguard and I am going to do this in a very committed heart, I will be dedicated and keep observing that Tanzania is benefiting to get all these.

Honourable Speaker, and my colleagues, I have an MBA in Finance. I am a Chartered Financial analyst in two different times. I have been trusted by two presidents. The late Dr. John Pombe Magufuli appointed me to be the District Executive Director for Magu District in Mwanza and then Her Excellence, Dr. Samia Suluhu Hassan appointed me to be the District Executive Director for Bukombe District in Geita. (Applause)

Honourable Speaker, I have a vast experience in private sector and I have worked for almost nine years in public sectors. So, I know I have what it takes one to be a key representative for this House in our country.

Dear colleagues, please, give me your yes votes is just adding value to your votes, adding value of representation of this house in our country. Please, I am kindly and humbly requesting your yes votes for me to be your representative. Thank you. (Applause)

SPEAKER: *Any questions?*

We go to the second candidate. Honourable Mwanahamisi Athumani Munkunda. (Makofi)

HON. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA: *Honourable Speaker, my dear Honourable Members of Parliament, my name is Mwanahamisi Athumani Munkunda, a Member of Parliament representing Special Seats from Shinyanga Region.*

I am a Member of Parliament, I am contesting representing you in the SADC Forum; and actually, we know that Tanzania plays a central role, strategic and historic in this Southern African Countries.

5 FEBRUARI, 2026

We know that Tanzania is acting as a bridge, as a key player in the development of regional politics, regional security and economic integration. (Applause)

Honourable Speaker, I am humbly asking you my member of Parliament, just to have your loyal vote for me to represent you. Actually, I will be your pioneer in promoting Tanzania as we know that Tanzania is a shining country in economic performance as it has a notable record in surplus of two billion threads, especially in export by using our ports and infrastructure. So, I will be there promoting using the infrastructure of Tanzania as a key and key player of these economic countries of the SADC.

Honourable Speaker, and my dear members, I will be enhancing the pace of economic cooperation, development and integration basing on the equity and mutual benefits of these countries as we know, we have to continue to promote the use of Swahili language as a product of our country.

Thank you, Members of Parliament, I humbly asking your votes for me to represent you in the SADC Forum. Thank you so much. (Applause)

SPEAKER: Any questions? Thank you very much.

Honourable Issa Mchungahela.

HON. ISSA A. MCHUNGAHELA: Honourable Speaker, thank you.

Thank you, my colleague, Members of Parliament. I go to the name of Issa Ally Mchungahela, Member of Parliament from Lulindi Constituent. I am contesting the position for SADC Forum Parliamentarian. Being a member of this very key decision making for the Africa in general, I will be most of representative who will give you some very good performance. I have a key performance relating to the vehicle. (Applause)

5 FEBRUARI, 2026

In fact, yes, in fact, as my name try to prevail; my name is Mchungahela that I am going to represent you for all financial matters because I am finance accountant and auditor international. Thank you. (Applause)

SPEAKER: *Any questions?*

Thank you very much. The last candidate is from the minority group, ACT-Wazalendo, Honourable Muhammad Alfani, yes, and we have Honourable Josephine Joseph Kapoma.

HON. JOSEPHINE J. KAPOMA: *Honourable Speaker, Honourable Members of Parliament, I stand before you this beautiful morning, to ask for your vote. My name is Josephine Joseph Kapoma, representing Women from Morogoro. I hold a Master's Degree from United Kingdom.*

(Hapa zoezi la upigaji kura wa Wajumbe wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) liliendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunakusanya kura.

Waheshimiwa Wabunge, ninaongeza muda mpaka tumalize shughuli ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wote tulishatumbukiza kwenye maboksi?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Haya fungeni.

Haya gaweni kundi la tano na la mwisho *Great Lakes*. Gaweni kundi la mwisho la Maziwa Makuu.

(Hapa zoezi la upigaji kura wa Wajumbe wa Umoja wa Maziwa Makuu (Great Lakes) liliendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kuna simu nyingine imepotea ya *Engineer Fatma*, tunaomba mtu ambaye ameiona ailete kwa Katibu hapa.

Haya kusanyeni.

Waheshimiwa Wabunge, wote tumeshatumbukiza kura zetu?

5 FEBRUARI, 2026

Hebu keti, nenda kwa Mheshimiwa Getere pale. Waheshimiwa Wabunge wote tumemaliza?

WABUNGE FILANI: Ndiyo.

SPIKA: Funga!

Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Tuna wagombea takribani 55, kwa mujibu wa taratibu zetu si busara watu 55 kwenda kusimamia kura maboksi matano. Ninawaomba wagombea, *options* mbili; kila kundi lichague mtu mmoja kusimamia boksi moja au tutafute Wabunge watano wakasimamie kuhesabu kura. (*Makofi*)

Kundi la Tume, *either* tumpate mgombea mmoja au tupate Mbunge aende akasimamie kura.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jesca Magufuli.

SPIKA: Nani?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Jesca Magufuli.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Khadija Aboud.

SPIKA: Subirini jamani. Umemtaja?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Jesca Magufuli.

SPIKA: Kwa upande wa Tume?

MBUNGE FULANI: Eeh, wa Tume. Naam! (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Jesca Magufuli, simama hapo, simama hapo hapo. Jesca simama hapo hapo. Inabidi lazima tuulize maswali; Kundi la PAP?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

5 FEBRUARI, 2026

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Aeshi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Asya Sharif. *(Makofi)*

SPIKA: Nani?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Saashisa Mafuwe.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Asya.

SPIKA: Mheshimiwa Mafuwe yupo?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Aeshi.

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Mafuwe. Simama hapo hapo. Kundi la SADC?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Aeshi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Taletale.

SPIKA: Mama uliyevaa nguo, dada yangu, Mheshimiwa unaitwa? Nani?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Aeshi.

SPIKA: Haya maboksi matano pelekeni huko. Mmeshafunga eeh?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Aeshi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Aeshi. *(Makofi)*

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Aeshi Kundi la SADC. Kundi la nne, IPU?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mary Chatanda.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Kafiti William Kafiti.

5 FEBRUARI, 2026

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mary Chatanda.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mary Chatanda.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mary Chatanda.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Babu Tale.

SPIKA: Mheshimiwa Chatanda umekubali? (*Makofi*)

MHE. MARY P. CHATANDA: Ndiyo!

SPIKA: Haya simama hapohapo. (*Makofi*)

Kundi la mwisho *Great Lakes*.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Kafiti William Kafiti.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Kijakazi.

SPIKA: Mheshimiwa Kafiti.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Kafiti William Kafiti. (*Makofi*)

SPIKA: Nimesimama. Waheshimiwa imekuja *note* hapa, kwa vile Mheshimiwa Aeshi ana mtu wake anagombea wamesema hafai kwenda kusimamia kura.

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Sanga.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Nancy Nyalusi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Kijakazi.

MBUNGE FULANI: Haidary Sumry.

5 FEBRUARI, 2026

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Sangu.

SPIKA: Mheshimiwa Haidary.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kijakazi.

SPIKA: Mheshimiwa Haidary Sumry, Meya.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Kijakazi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Nancy Nyalusi.

SPIKA: Waheshimiwa tumeshapata wawakilishi watano.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Nancy Nyarusi.

SPIKA: Tumeshapata wawakilishi watano. Sasa ombi langu kwenu, kura hizi zitachukua muda kuhesabu. Tuwaache wahesabu kura, matokeo tutangaze jioni, sababu tayari tuna wawakilishi wetu.

WABUNGE FULANI: Sawa. *(Makofi)*

SPIKA: Tumekubaliana?

WABUNGE: Ndiyo.

SPIKA: Matokeo yatatangazwa jioni, Saa 11.00. Tunao mawakala, maboksi yametoka hapa yamefungwa.

Mawakala njooni msimame hapa. Waheshimiwa Mawakala tazameni hivi, tazameni huku.

Waheshimiwa Wabunge, mbona mmekuwa wengi? Sita! Wanatakiwa watano, mbona mko sita?

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo.

5 FEBRUARI, 2026

SPIKA: Haya, haina neno, wanaweza kwenda wote, haina neno. Jamani mawakala wetu ndiyo hawa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, aende Mheshimiwa Bashe. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Mawakala wetu ndiyo hawa. Mheshimiwa Magufuli nyanyua mkono wakutambue. Mheshimiwa Jesca Magufuli usinitazame mimi, watazame wao, watazame huko, siyo mimi. Mheshimiwa Jesca Magufuli, Mheshimiwa Haidary, Mheshimiwa Mafuwe, Mheshimiwa Chatanda. *(Makofi)*

Sasa na dada yetu uliyevaa nguo ya wananchi, unaitwa Asma eeh, Mheshimiwa Asma?

WABUNGE FULANI: Ni Mheshimiwa Asya.

SPIKA: Mheshimiwa Asya, Mheshimiwa Asya Sharif?

Haya, ninaomba sasa tuelekee chumba cha kuhesabia kura. Piteni huku.

(Hapa Zoezi la Kuhesabu Kura zilizopigwa lilifanyika)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza ninawashukuru kwa utulivu na kumaliza zoezi letu kwa ukamilifu. Makundi matano yote yatatangazwa Saa 11.00 na utaratibu wa kutangaza tutaambiana hapa Saa 11.00.

Sasa ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 Jioni.

(Saa 7.10 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

5 FEBRUARI, 2026

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI: Kamati ya Mipango.

NAIBU SPIKA: Kamati ya Mipango

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

**Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda mrefu 2026/2027 -
2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo
wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031) na Mapendekezo
ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa
kwa Mwaka 2026/2027**

na

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango
na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya
2026/2027 - 2028/2029**

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tunaanza na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, atafuatiwa na Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi na Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, ajiandae.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kwenye mapendekezo yaliyowasilishwa Mezani na Waziri.

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka miaka 49 iliyopita tarehe 5 Februari, kilizaliwa chama maarufu sana duniani, kinaitwa Chama Cha Mapinduzi na kwa hiyo, leo kinatimiza miaka 49, ninaomba kuanza kwa kukitakia chama changu *happy birthday*. Kimefanya mengi kwa nchi yetu, vimebaki vyama vichache kama hiki, kwa hiyo wana-CCM wana kila sababu siku hii ya leo tunapokumbuka kuzaliwa kwa chama hiki, kutembea kifua mbele kwa sababu tumefanya mengi, nchi yetu inaendelea kuwa na utulivu. Niwapongeze viongozi ambao wanatuongoza, wakiongozwa na Mwenyekiti wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, wanakiongoza vizuri chama hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni chama kinachoongozwa na wanadamu kinaweza kuwa na misukosuko, kina milima na mabonde. moja ya siri ya uimara na uthabiti wa chama chetu ni uwezo wetu wa kujikosoa na kukosoana. Hili limekuwa ni msingi mkubwa wa chama chetu na ninaamini tutaendelea nalo ili tuweze kuboresha kadri mambo yanavyoenda. Mwalimu alituambia kujikosoa na kukosoana ni silaha ya mapinduzi kwa hiyo, *happy birthday* kwa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kizalendo wa kuendelea kuiunda Wizara ya Mipango na tumeendelea nayo na ninaamini inatupa matokeo ambayo yanatupa faraja Watanzania. Nimpongeze kwa kuendelea kumwamini Profesa Kitila Mkumbo, mtu maarufu, mtu mwema, hodari na mzalendo sana. Profesa pamoja na timu yake ndiyo maana wamefanikiwa kwa uthabiti na uhodari mkubwa kutuletea Dira ya Mwaka 2050 na sasa wametuletea Mpango Elekezi wa Muda Mrefu, Mpango wa Kati na Mpango wa Muda Mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyenzo ambazo huko nyuma hatukuwa nazo na ndiyo maana matokeo hayakuwa mazuri, kwa hiyo nimesimama kumpongeza Profesa Kitila na watu wako kwa jambo hili jema ambalo wamelifanya na kwa kweli tunamrudishia heshima Rais wetu, kwa kuamini kwamba mipango ndiyo msingi wa maendeleo yetu. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kwamba tumepata dira, tumepata hizi *documents* tatu muhimu sana katika utekelezaji, sina mashaka kwamba dira itatekelezeka, lakini ninataka kupendekeza mambo machache:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ili hii dira itekelezeka tuna eneo moja muhimu tukalimalizia, wameanza nalo vizuri kwenye taasisi za umma, kuwapata viongozi watacaoongoza taasisi za umma na bodi zao kwa uwazi, lakini na mpango wa kusaini mikataba ya matokeo, kwa maana ya *contract of performance*. Ni kwamba, mtu akiwekwa mahali apewe malengo, asipoyatimiza kusiwe na mjadala wa yeye kuendelea kuwa pale, aondoke tuweke mtu mwingine mambo yaende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kupendekeza twende mbali zaidi, twendeni na kwa watumishi wa umma wale wenye *level* ya uongozi, kwa maana ya Maafisa Waandamizi, Wakurugenzi na Watendaji Wakuu. Tumekuwa na utaratibu watu wakishapewa wanabweteka mpaka wanastaafu hata kama hawatakuwa na matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani ili mpango huu uende vizuri, ninamwomba Profesa Serikalini wafanye uamuzi, hawa watendaji wa umma nao tuwape mikataba ya utekelezaji ambayo ndani yake itakuwa na malengo, tutayapima kwa muda mfupi na muda mrefu na kama mtu hafanyi tusimung'unye maneno, akae pembeni tuweke wengine, tutasonga mbele. Tukiweka huu utaratibu kwamba nikishakaa nitakwenda mpaka nitastaafu, tutapiga *mark time* na kazi hii nzuri waliyoifanya haitakuwa na matokeo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; nimependa tumekuja na hii dhana ya kutotekeleza mradi mmoja mmoja unavyojitegemea wenyewe. Tumekuwa na miradi ya mfano, lakini wamekuja na programu ya miradi mbalimbali, kwamba, tunakuwa na mradi mkubwa na ndani yake kuna miradi ambayo inategemea au inategemeana na huu mradi mkubwa katika utekelezaji. Hili ni jambo zuri nimeona hapa wameleta programu ya miradi saba, ndani yake kuna miradi shikizi 45, hili ni jambo zuri, litaongeza kasi ya ukuaji wa

5 FEBRUARI, 2026

uchumi wetu na litasaidia tupige hatua kwa kasi zaidi. Hili ni jambo zuri na ninaamini lisimamiwe litekelezwe sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ninataka kupendekeza. Katika zile programu saba walizonazo tunayo programu moja ya mradi wa kuchakata gesi asilia wa Lindi, katika mradi huu ndani yake kuna miradi shikizi mitatu, barabara ya kwenda Kusini, kuna bomba la gesi pia kuna mafunzo maalum kwa taaluma itakayotumika kwenye mradi huu. Ninaomba kupendekeza, tuongeze mradi mmoja shikizi kwenye hii programu ambao ni Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa kutoka Dar es Salaam – Lindi kwenda Mtwara na nitatoa sababu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza, *concept* ya kuunganisha bandari, ujenzi wa reli unaunganisha bandari na bandari. Hapa tunayo Bandari ya Dar es Salaam, tunayo Bandari ya Uvuvi ya Kilwa, tunayo Bandari ya Lindi, tunayo Bandari ya Mtwara. Kwa hiyo reli hii inaziunganisha hizi bandari zote, itasaidia uchukuzi wa mizigo na abiria, Pia reli hii itakwenda kutuunganisha na reli wanayoiita ya Kusini, reli ya kutoka Mtwara kwenda Mbamba Bay, kwa sababu ume-*hang* peke yake, tuiunganishe na Bandari ya Dar es Salaam, itatusaidia mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mradi shikizi kwa mradi wa gesi kwa sababu huu mradi wa gesi mkubwa ni wa dola bilioni 42, siyo mradi mdogo, hakuna mradi unaoufikia kwa gharama yake, lakini ujenzi wake utatuchukua miaka saba. Wakati wa ujenzi tutaingiza mitambo hapa nchini, mingi itapitia Bandari ya Dar es Salaam, inafikaje Lindi? Ndiyo maana nikasema ninadhani vizuri katika miradi ile mitatu tuongeze mradi wa nne tuwe na Mradi wa Reli ya kisasa inayotoka Dar es Salaam, inapita Kilwa unaongeza thamani ya Bandari yetu ya Uvuvi ya pale Kilwa, unaingia Lindi na wakati wa kurudi tuna mizigo wa *cement* ya Dangote na kadhalika. Ninaomba Profesa ufikirie tuongeze kwenye miradi shikizi katika programu hii kubwa ya Mradi wa *LNG*. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne; hii miradi ukiangalia imepangwa vizuri sana, imetawanywa mahali kwingi na ina fedha nyingi na ninafurahi kwamba wanakubali itaendeshwa kwa sehemu kubwa na *private sector*, lakini *private sector* ambayo haijaandaliwa na haijaandaliwa kwa makusudi na Serikali haitaweza kushiriki kwenye hii miradi, matokeo yake hizi fedha zitakwenda nje. Kwa hiyo, ninataka kutoa wito kwa Serikali, wasikwepe wajibu wa kuiandaa *private sector* kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye huu Mradi wa Lindi na wakati wa kampeni alipokuja mgombea Urais tulimwambia, tunapendekeza VETA za Kusini zitengeneze programu maalum ya kuwa-*train* mpaka watoto wa darasa la saba, watoto wa *form four* na kadhalika, waende kuhudumia kwenye gesi hii, tusipowaandaa mpaka walinzi watatoka nje ya nchi na hii ni wajibu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata *private sector* yenyewe Serikali ndiyo ambao wanajua fursa zipo wapi, wasipokaa nao wakadhani wataona wenyewe, *private sector* za wenzetu tunazoona zimeendelea zimeandaliwa, kuna mkono wa Serikali kwenye ujuzi, kwenye fursa pia kuwawezesha kupata mitaji. Tusione aibu, tuiwezeshe *private sector* ishiriki, ninadhani hili kubwa sana. Tukifanya hivi kwenye miradi yote hii fedha haitaenda nje, itabaki hapa ndani na tutashuhudia maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niendeleo suala la tano. Wakati tunaomba kura...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, malizi malizia hoja ya mwisho maana muda umesogea.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika mbili za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaomba kura, tulikuwa na kauli mbiu kwenye kampeni yetu "KAZI NA UTU," kauli hii haikuja kwa

5 FEBRUARI, 2026

bahati mbaya. Katika imani tatu za Chama Cha Mapinduzi mojawapo ni utu wa binadamu, kwa hiyo haikuwa bahati mbaya. Ninataka kukiomba chama changu, kuanzia mwanzo hapa tunapoanza mipango ya utekelezaji wa dira hili suala la “utu” liwe wazi, tulione moja kwa moja kwenye mipango ya Serikali. Tukienda kwenye machinga tuone utu, tukienda kwa wakulima tuone utu, tukienda kwenye matendo ya vyombo vya dola tuone utu, tukimung'unya maneno CCM itaondoka jamani! Tulisimamie suala la utu liwe sehemu ya *culture* yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu alituambia, Serikali kwa asili yake ni chombo cha mabavu, wanaoweza ku-*regulate* hili ni chama kupitia Bunge, Mabaraza ya Madiwani lakini na vikao vya chama vyenyewe. Ninataka kuwaomba Wana-CCM tusimung'unye maneno kwenye suala la Serikali kuthamini utu wa binadamu, kwa sababu ndiyo imani ya chama chetu na tusione aibu kuisimamia macho kwa macho ili tusonge mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji ajiandae.

MHE. MUHSIN HAJI USSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwa heshima kubwa ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambaye ametujalia tumekuwa hapa Bungeni tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninaomba kwa heshima kubwa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ushindi mkubwa wa kishindo alioupata katika uchaguzi wa tarehe 29 Oktoba, 2025. Sambamba na hilo ninampongeza sana Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa ushindi mkubwa wa kishindo kule Zanzibar. (Makofi)

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine nikishukuru sana chama changu, Chama Cha Mapinduzi kwa kunipa heshima ya kupendekeza jina langu na kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Malindi kunipigia kura nyingi za kishindo na leo nimesimama kijana wao nikiwa ni Mbunge ambaye siku zote nimeahidi kuwa sauti ya Wanamalindi na kuhakikisha Jimbo la Malindi linapata mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye amepata fursa ya kuaminiwa na Mheshimiwa Rais, lakini niwapongeze Wabunge wote ambao Chama Cha Mapinduzi kimeona sisi tunafaa kuwa wawakilishi katika maeneo yetu. Kwa hili nimpongeze sana Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa na Imani na sisi na ninaomba tumpigie makofi mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilibahatika kupata nafasi ya kuipitia hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, ambayo imeelezea Mpango Elekezi wa Muda Mrefu, Mpango Elekezi wa Miaka Mitano na ule wa Mwaka Mmoja. Ukiangalia dhima na malengo ya Mpango wa Nne hasa wa kipindi hiki cha miaka mitano unaeleza kwamba ni kuwa na mageuzi kwa ajili ya ukuaji wa uchumi jumuishi na uzalishaji wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niunge mkono jambo hili lakini, vilevile nikiwa kama kijana tunapozungumzia mageuzi kwa ajili ya ukuaji wa uchumi, uchumi shirikishi, uchumi jumuishi, uzalishaji wa ajira na ukuaji wa pato la Taifa ni lazima tukubaliane jambo moja ambalo ni la msingi sana. Hakuna nchi yoyote duniani inayotegemea kuongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi yake kwa kutumia zaidi kuliko kuzalisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nchi nyingi zilifanikiwa na sisi Tanzania kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa, lakini lazima tukubali kubadili baadhi ya sera za nchi yetu. Hii tukubaliane uchumi wa kuzalisha ndiyo uchumi ambao unasaidia kukuza ajira kwenye nchi yetu na uzalishaji huu, ni lazima bila kupepesa macho tuwashirikishe vijana ambao ndiyo nguvukazi na injini ya Taifa letu. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, Nchi ya Nigeria, walipoamua kulinda uzalishaji wa mpunga ndani ya nchi yao, walipoamua kulinda viwanda vinavyochakata mpunga na kutoa mchele kwenye nchi yao kwa makusudi vilitoa nafasi ya viwanda hivi kukua na kutoa fursa kwa vijana kujishirikisha moja kwa moja kwenye kilimo chenye tija na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unazungumzia kwa takwimu za mwaka 2024 zaidi ya 75% Nchi ya Nigeria wanatumia mchele wao wenyewe. Hii ni kwa sababu walikubali kubadilisha sera zao. Sasa kama vijana ni kipi tunaishauri Serikali? Serikali iangalie namna bora ya kupunguza tozo kwa viwanda ambavyo vinaongeza thamani ya mazao yetu. Hapa ninaipongeza Serikali, tulienda maeneo ya Kusini kule Lindi na Mtwara tunapata somo hapa, pale tulipoanza kuhakikisha kwamba, zao la korosho lazima lianze kuchakatwa likiwa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliona ajira ziliongezeka na korosho zimeongezeka thamani. Leo vijana wa Kitanzania wanapata fedha nyingi kuipitia korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuwa na elimu na mafunzo yanayolenga ajira. Tatizo letu sisi Watanzania si kwamba hatujasoma na si kwamba vijana hawana elimu, bali mara nyingi hawasomei kile ambacho soko linahitaji. Kwenye hili nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mimi ni miongoni mwa vijana ambao wamebahatika kutembea mikoa yote Tanzania; kila mkoa, kila wilaya, Serikali imewekeza fedha nyingi kwa kujenga miundombinu bora ili kuwapatia elimu vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukienda Ujerumani leo, Ujerumani wamefanikiwa kwa namna moja kupunguza changamoto ya ajira kwa vijana. Hakukuwa na miujiza bali walitumia mfumo unaoitwa *dual training*; mwanafunzi anasoma na wakati huo huo anapata uzoefu wa kufanya ajira katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, sasa tuishauri Serikali, ufike wakati tuone namna bora ya kuwashirikisha wanafunzi katika ajira, wanapotoka wamepata uzoefu. Kampuni mbalimbali ziwachukue vijana hawa wawafundishe na

5 FEBRUARI, 2026

wawe wanawapa malipo. Tuangalie namna ya kuzipunguzia baadhi ya tozo ili kampuni hizi ziweze kufanya hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mifano hai, ukiangalia wanafunzi waliomaliza VETA waliosomea ufundi wa umeme, *welding*, ujenzi hawa wakiingia mtaani hawapati shida kutafuta ajira na kuajiriwa kwa sababu amesoma kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu ameendelea kuweka mkakati wa kujenga VETA nchi nzima katika kila wilaya. Serikali inafanya vizuri, lakini tunaomba tuwashauri kufanya vizuri zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ninataka nizungumzie kidogo kuhusu kilimo cha kisasa. Kilimo kisionekane kwamba ni sekta ya umaskini, kilimo ni fursa ya biashara. Hapa Tanzania ukienda maeneo ya Kilombero, ukaenda Mbarali Serikali imewekeza vizuri katika njia ya umwagiliaji, niipongeze sana Serikali yetu. Kwa hiyo, tukifanya hivi tukizalisha viwanda vidogo vidogo vitakua na ajira zitaongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Bangladesh mamilioni ya vijana wameajiriwa katika viwanda vya kutengenezea nguo. Tuna mifano hapa, ukienda Singida viwanda vya alizeti vimeajiri vijana wengi, hata hapa Dodoma vimeajiri vijana wengi. Tunaishauri Serikali kuhakikisha ya kwamba wanapanua *industrial parks* katika mikoa na kufikisha huduma zote muhimu ikiwemo barabara, umeme wa bei nafuu na maji ya kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia kutokana na muda; tuwe na mitaji rafiki kwa vijana. Vijana wana mawazo, utayari na uthubutu. Changamoto ya vijana ni kwamba, wamekosa mitaji na fedha. Niipongeze Serikali yetu, Mheshimiwa Rais amehakikisha 10% katika kila halmashauri mapato yake yanatengwa ili kuwasaidia vijana kuwapa mikopo akinamama na wenye mahitaji maalum. Vijana wanapata 4%, lakini tujiulize takwimu zinaonesha zaidi ya vijana milioni 24 wameshapata fedha hizo. (Makofi)

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajitahidi sana kuhakikisha ya kwamba inatoa *input* ambayo ni *capitals*. Serikali inafanya kazi ya kutoa *output* ambayo ni kuwapa mikopo hao. Wapi tunakwama? Tunakwama kwenye *outcomes* na *impact*. Hatuoni hiyo mikopo inafanya *activities* gani ambazo vijana wanaweza kuonesha? Hatuoni *economic growth* ya vijana ni ipi? Leo tujiulize kijana tuliyemkopesha alikuwa na uwezo wa kuingiza shilingi 500,000 kwa mwezi, je, leo na uwezo wa kuingiza 2,000,000 kwa mwezi? Kijana huyo anaweza kujijengea nyumba yake na kusaidia familia yake? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai na hasa kwa Wizara ya Vijana, kaka yangu Mheshimiwa Joel Nanauka tuangalie namna gani *outcome* na *impact* kwa mikopo ambayo vijana wanapatiwa ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa muda umekwisha.

MHE. MUHSIN HAJI USSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme, ninaunga mkono hoja na Serikali tunaipongeza kwa kazi kubwa inayofanya kuwaletea maendeleo wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa, Dkt. Selemani Saidi Jafo, atafuatiwa na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, ajiandae.

MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametuendesha na mchakato wetu huu ambao tunaendelea nao. Pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Kupitia vyombo ya habari tunaona Mheshimiwa Rais anavyofanya *resource mobilizations*. Yuko kule Falme za Kiarabu katika mikakati mipana ya kuhakikisha kuwa nchi yetu

5 FEBRUARI, 2026

inasonga mbele. Hongera sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii nimpungeze kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa mpango huu mzuri aliokuja nao na *documents* zote kwa ujumla wake na shemeji yangu pale Mheshimiwa Naibu Waziri. Hakika timu imetulia vizuri, hatuna mashaka kwamba kazi hii itaendelea kufanyika vizuri. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ni mtu rahimu sana, ni mtu anayesikiliza sana. Amepewa kijana *very aggressive, very innovative*; Mheshimiwa Dkt. Chaya. Sina mashaka nchi yetu inakwenda sehemu salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia masuala funganishi kwanza. Ukiangalia mpango huu na *documents* zote kwa ujumla zinazungumzia jinsi gani tutatengeneza uchumi wetu; lakini malengo makubwa tufike dola za Kimarekani trilioni moja ifikapo 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujielekeza katika upande wa utalii. Katika hili niombe sana tuweke mikakati ya kutosha, tusiwe nchi ambayo kwa kiwango kikubwa tunategemea utalii wa Kaskazini pekee yake, haiwezekani. Ninadhani hili tuliangalie vizuri. Katika maelekeo haya mapana na hasa ukiangalia *Royal Tour* ambayo Mheshimiwa Rais alifanya imesaidia kufungua uchumi kwa kiwango kikubwa. Tusukume utalii wa Kaskazini, lakini kule Katavi, watu wa Mtwara na maeneo mengine yote utalii ufunguke, uchumi utengenezeke vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nilitaka kuchokoza jambo hilo kwa sababu kuna eneo linaitwa *Nyerere National Corridor* ambalo hili ni jina la Kizaramo kule, utaenda kulitafuta; linaanzia *Airport* linapita Kisarawe mpaka katika Bwawa la Nyerere. Katika hili ninashauri; kwamba mipango hii iangalie jinsi gani itafungua *corridor* hiyo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mtalii akishuka Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam kwenda katika Hifadhi ya Nyerere atahitaji muda wa saa moja na nusu endapo ile barabara itakamilika.

5 FEBRUARI, 2026

Barabara hiyo ina wastani wa kilometa 150 pekee yake. Siyo suala zima la utalii pekee yake, lakini tuna *investment* kubwa ya Bwawa la Nyerere ambalo linatakiwa lilindwe. Hata *emergency* ya aina yoyote ikitokea lazima watu waende kwa haraka; hiyo ndiyo *shortest road*. Niombe tuliangalie kwa upana wake na hasa ujenzi wa barabara ukamilike kwa kiwango cha lami kwa haraka zaidi. Lengo kubwa ni kwamba tutatengeneza uchumi wa utalii pamoja na kulinda rasilimali zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana kuhusiana na mpango huu na hasa uwekezaji mkubwa ambao tunatarajia kuufanya; kaka yangu Mheshimiwa Nape amezungumza pale. Mradi wa gesi ndiyo *game changer* wa nchi hii. Mradi huu wa *investment* ya Dola za Kimarekani bilioni 42 itabadilisha mtazamo wetu Watanzania wote. *Contribution* yake *annually* kati ya Dola bilioni tatu hadi bilioni sita kwa mwaka; katika *GDP* itaongeza kati ya Dola za Kimarekani bilioni 200 hadi bilioni 300. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili maana yake ni nini? Maana yake niombe sana Tume ya Mipango, Wizara ya Mipango kwa ujumla wetu mradi huu tuuweke kipaumbele; tuseme sasa *enough is enough* mradi uanze. Hii itasaidia ku-*unlock* na kupeleka mbele uchumi wetu. Tukifanya hili tutakuwa tumefika mahali pazuri zaidi. Nimefurahi mradi huu upo, lakini niombe sana sasa, ikiwezeka tutengeneze kabisa utaratibu mzuri wa jinsi gani mradi huu uanze haraka ili kubadilisha uchumi wa nchi yetu na ili tufikie malengo yale tunayoyataka. Ikifika mwaka 2050 tuwe na huu mradi ukiwa umekamilika na unafanya kazi; hali kadhalika kuhakikisha kwamba uchumi wetu unafikia *GDP* ya kuwa trilioni moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ambao umezungumza kwa muda mrefu sana Mradi wa Mchuchuma na Liganga. Wenzangu wa Ludewa na Njombe wamezungumza sana mradi huu. Niishukuru sana Serikali, kazi kubwa imeendelea kufanyika katika mradi huu. Ninajua kuwa hatua sasa zimefika mahali pazuri na muda si mrefu mradi utaanza. (Makofi)

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuombe kwamba tuhakikishe mradi huu tuusimamie vizuri, utabadilisha uchumi huu. Viwanda vyote vya chuma vitategemea Mradi ule wa Mchuchuma na Liganga. Tunahitaji tuzalishe magari nchini mwetu, gari hatuwezi kuzalisha bila kuwa na chuma. Kwa hiyo, niombe sana; mradi huu upo na bahati nzuri Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ameuweka vizuri katika *document* hizi. Tuombe sasa tuweke utaratibu vizuri ili tuhakikishe kuwa wenzetu wa Ludewa, akina Mheshimiwa Kamonga na wenzake waweze kupata mafanikio makubwa kupitia mradi huu, ambao ni matarajio ya Watanzania katika kutengeneza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watani zangu humu, Wasukuma na Wanyawezi. Hawa tangu wanazaliwa wanalima pamba, hawana lolote wanalofikiri, ni pamba. Ninaomba, kipindi hiki cha utekelezaji wa mpango huu tuanze kuhakikisha kuwa tunakuja na ule mpango wa *cotton to cloth*. Vilevile tuwezeshe viwanda vya nguo; na viwanda hivi ili tuviwezeshe ni lazima tukubaliane kama nchi tupunguze gharama za umeme katika viwanda vya nguo ili mradi uweze kufanya kazi. Tuweke *special incentives*, kwamba atakayeweka kiwanda cha nguo basi kiwango cha umeme kitashuka. Lazima tu-*sacrifice* kama nchi ili kuhakikisha kuwa tunasonga mbele katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie, endapo tutafanya hilo viwanda vingi sana vya nguo vitakuwepo hapa na watani zangu niliowasema, hawa wanaolima pamba, Wanyamwezi na Wasukuma watakuwa na uhakika wa kilimo chao na hatutaona pamba inayosafirishwa inaenda nje, tutakuza uchumi wa nchi yetu. Kubwa zaidi, duniani viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi zaidi ni viwanda vya nguo. Leo hii nenda pale Morogoro, kiwanda kimoja zaidi ya watu 3,000 wapo pale ndani. Tukifanya hili tutafikia malengo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana kutokana na suala la *modernization* ya miji yetu. Niombe, jambo la kwanza; leo hii tunafanya kazi kubwa katika Jiji la Dar es Salaam katika kutengeneza barabara za mwendokasi. Niombe Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwezekana itengeneze timu maalum itakayohusisha Wizara kadhaa; Wizara ya

5 FEBRUARI, 2026

Mipango ikiwepo, Wizara ya Maji ikiwepo, Wizara ya TAMISEMI na nyingine. Zile barabara; twendeni sasa hivi Ethiopia, Addis Ababa; barabara tumetengeneza nzuri, twende tukazilinde barabara zile; tufanye *beautifcation* ya Dar es Salaam yetu. Tuna AFCON inakuja mwakani hapa tutengeneze Dar es Salaam ipendeze zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nifurahi sana, twendeni tukaanze na zile kata nyingine za Dar es Salaam kwa ndugu zangu, Wazaramo wenzangu wa Vingunguti, Buguruni kule Tandale na maeneo mengine. Twende tukafanya *situation incentives*, tuvunje yale maeneo, tuwalipe fidia watu, tujenge magorofa na tuwape na *apartment* ili mtu asione shida kutoa eneo lake. Jambo la kwanza, anapata fidia lakini pia ghorofa likijengwa anapata *apartment* moja. Hii italibadilisha Jiji la Dar es Salaam lote, hivyo ni lazima mji upendeze. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine walipata changamoto kubwa wananchi wanalalamika, sisi twende na model tofauti tofauti. Mtu alipe fidia, jengo lijengwe refu na kubwa halafu anapewa *floor* moja. Naye atajivunia kuwa anatengeneza uchumi wa nchi yetu. Niombe sana ikiwezekana jambo hili lianze haraka; kwa sababu sasa hivi Dar es Salaam imekuwa ni sehemu ya kivutio kikubwa, ni lazima tuliweke vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukienda kwa SGR ukifika pale Kipawa unanza kufunga viatu unaogopa kuangalia nyumba za pembezoni, ni lazima tuzibadilishe zile. Tuzibadilishe na kuwasaidia wale wananchi wapate kipato kizuri, wawe na uhakika kuwa wanalipwa fidia na pia majengo yakijengwa wanapata *floor* moja ya kuishi, wajivunie maeneo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, lakini si kwa umuhimu nipendekeze, ikiwezekana tuanzishe utaratibu wa kuwa na *Industrial Bank* ambayo itawasaidia wale wawekezaji katika upande wa viwanda. Kuwa na benki maalum inayowasaidia kupata fedha ya kufanya uwekezaji. Tunapokwenda katika ajenda ya viwanda ni lazima tuwe na mikakati mikubwa ya kusaidia viwanda hivi. Lazima

5 FEBRUARI, 2026

tuwe na benki ambayo itasaidia msukumo wa kibiashara katika upande wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache ya siku ya leo, nikushukuru sana. Niwashukuru Wajumbe hawa wa jengo hili lote kwa zile kura walizopiga. Hatujui matokeo yatakuwaje lakini ninasema ahsanteni sana kwa niaba ya wenzangu na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo. Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, ajiandae.

MHE. ARIF S. PREMJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, niwapongeze sana Mawaziri wetu na Manaibu wetu kwa kutuletea Mpango wa Mwaka Moja, wa Miaka Mitano na wa Miaka 2025. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais ambaye yupo kwenye *World Government Summit*. Anatuwakilisha vyema na anatusemea vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina hekta milioni 44 kwa ajili ya kilimo; na ndani ya hekta hizo tuna hekta milioni 29 ambazo ni za umwagiliaji. Hivi hapa tunapozungumza hata hekta 1,000,000 hatujacross. Kwa hiyo, tuna kazi kubwa sana ya kuhamasisha ili tuweze kufikia lengo hilo la trilioni moja baada ya miaka 25. Kwa nini, nime-*highlight* hiyo; ni lazima tuwe na malengo, kwamba ndani ya mwaka fulani tufikie kwenye hekta kadhaa ndani ya mwaka fulani tufikie kwenye hekta kadhaa na tufikie hapa. Ni lazima tuwe na *key performance indicator* ndiyo itatu-*guide*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mpango wa mwaka moja; na hili ni pendekezo kutoka kwa wananchi wa Mtwara Vijijini, ninaomba niliweke wazi kabisa. Mwaka 2013 palikuwa na misukusuko mingi sana ya gesi itoke, isitoke, kwa kuwa wananchi wa Mtwara walikuwa wanahisi kwamba ikitoka hawatanufaika. Serikali ya Mheshimiwa Rais imefanya jitihada kubwa, wananchi sasa hivi wananufaika vizuri. Tulipata Kituo cha Afya pale Msimbati, lakini

5 FEBRUARI, 2026

sambamba na hilo tuliwekewa na mashine mbili za kufua umeme kwa kutumia gesi za megawati 40. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa unyenyekevu mkubwa wanaomba Barabara ile ya Ziwani – Madimba – Msimbati; na Madimba – Tangazo – Kilambo, kwa kuwa wanatambua kwamba gesi inachangia kwenye pato la Taifa takribani shilingi milioni 100. Takwimu hizo zipo kwenye NBS (*National Bureau of Statistics*) za mwaka 2024. Hilo ni pendekezo la kwanza kutoka kwa wananchi wa Mtwara Vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango iliyopo ni mizuri. Mara nyingi huwa ninaona changamoto mbili; ya kwanza maamuzi na ya pili ni muda mrefu wa maamuzi. Hapa ninaomba ni-*highlight*; leo hii Mradi ule wa LNG ulikuwa kipaumbele cha Taifa kuanzia mwaka 2014. Tunavyozungumza sasa hivi ni siku 4,380 bado tupo kwenye majadiliano, hatujasaini *host government agreement*, hatujasaini *product sharing agreement* na wala haijafika *final investment decision*. Ukiangalia upande wa pili, tukivuka tu, Msumbiji, wenyewe by 2029 watakuwa wameshaingia kwenye soko la kimataifa. Kwa hiyo, tuangalie *factor* ya muda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hilo tu, 2022 wakati ule alikuwepo Mheshimiwa Makamba; na kwenye bajeti palikuwa na Mradi mwingine wa Bomba la Gesi kusambaza kwenda kupeleka Uganda na Kenya pia na bajeti zilikuwa zime-*set*; takriban shilingi bilioni 656 kwenda Kenya na shilingi bilioni 635 kwenda Uganda. Kwenye kutekeleza maamuzi; leo hii kama tungetekeleza ule mradi tungekuwa tunauza gesi nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo, *potential* ya gesi bado hatujaitumia vizuri. Juzi kati niliona kwamba tunafanya mazungumzo na *Lock Country Mountain* ya Canada kwa mradi wa Dola za Kimarekani milioni 420; mradi ambao *uta-convert gas into liquid* ili kupata *diesel* na *jet fuel*. Hii miradi ya kimkakati ifanye kazi sasa hivi. Siyo hilo tu, Serikali yetu ilisaini MoU na Kampuni ya ESA ya Indonesia, bado utekelezaji. *Factor* yangu ni moja tu, *time* inatugharimu kwenye *ku-make decisions*.

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu hivi vikiharakishwa, tukaenda na muda, tukafikia *end point* ni lazima tutafanikisha kwenye mipango yote ya miaka 25. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Wabunge waliopita kupitisha ile sheria ya *Tanzania Investment and Special Economic Zone Act* ya 2025 ambayo dhana na dhamira yake ilikuwa ni kuhamasisha uwekezaji, lakini sambamba na hilo kuwezesha uwekezaji. Kwa hiyo nisisitize sana hilo. Hayo maandishi ya kisheria yapo kwenye makaratasi yaje kwenye uhalisia. Lazima kile ambacho tunachoki-*preach* sasa tuki-*practice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa sina mengi sana, kwa faida ya muda ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Premji kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sana kwa kumpongeza Waziri wa Mipango na Naibu wake kwa wasilisho zuri sana la mipango yetu, (Mpango wa Muda Mrefu, Mpango wa Muda wa Kati na Mpango wa Muda Mfupi). Ni mipango ambayo kwa kweli ni mizuri na kama tutaisimamia na tutaitungia sheria ya kuitekeleza inaweza ikatuwezesha kufika pale ambapo tunatamani kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili; nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuja na mwongozo wa upangaji wa bajeti mzuri sana ambao kwa leo sitokuwa na *comment* katika eneo lake hilo kwa sababu ni mpango mzuri sana ambao umekuja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; nipongeze taarifa ya Kamati ya Bajeti, taarifa nzuri sana. Kamati wamedadavua na wamechambua vizuri, nina imani kabisa mapendekezo haya yakifanyiwa kazi yatasaidia sana katika kuboresha mipango yetu na kuipeleka nchi mahali pazuri. (Makofi)

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii ambayo tumeisema, ukiiangalia na kuisoma unaona namna Serikali inavyopambana katika kuhakikisha kwamba tunapambana na maadui, maadui wakubwa wa Taifa letu ambao wamekuwa ni kero katika maeneo mengi. Maadui hao ni umaskini mkubwa ambao upo katika Taifa letu ambao unawakabili wananchi. Karibu zaidi ya robo ya Watanzania ni maskini. Sasa mipango hii inatupeleka kwenda kukabiliana na umaskini huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni ukosefu wa ajira na la tatu ni ukosefu wa maarifa na ujuzi wa kutosha wa wananchi wetu ambao tunaita kwamba tunakuwa na ujinga kwa sababu hatuna maarifa ya kutosha. Rasilimali zipo za kutosha, lakini uwezo wetu wa kuzitumia katika kuzibadilisha na kuleta maendeleo bado ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni uchumi mdogo na ukuaji wa uchumi mdogo wa nchi yetu. Ninaomba nianzie hapa kwenye ukuaji wa uchumi. Dira yetu wameitengeneza vizuri sana Profesa na kwa kweli inavutia, kwamba ifikapo mwaka 2050 tuwe tumefikia pato la Tanzania inayofikia dola za Marekani trilioni moja. Kwa kweli kulitamka ni rahisi sana, lakini kulitenda, kwenda kufikia maana yake lazima tujipange sawasawa ili tuweze kufikia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye uchumi sasa hivi kwa mwaka mmoja inaonekana unatarajiwa kukua kwa asilimia sita. Sasa ukuaji wa asilimia sita, hautatupeleka kufikia kwenye pato hilo. Kwa hiyo, lazima mipango yetu sasa tuidadavue vizuri, ituondoe kwenye ukuaji wa asilimia sita twende kwenye ukuaji wa uchumi wa asilimia zaidi ya 12, ndipo tunaweza tukafika kwenye hilo pato ambalo tunalitamani kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema ukuaji wa asilimia sita au ukuaji wa 12% lazima tuziweke vizuri sekta zote na tuweke shabaha zake. Tuoneshe sekta za uzalishaji zitachangia asilimia ngapi, sekta za huduma za jamii zitachangia kwa asilimia ngapi. Kila sekta tuweke shabaha wazi wazi kusudi kila mwaka tuwe na uwezo wa kujipima kuona kwamba hii sekta imefika kwenye shabaha tuliyopanga au

5 FEBRUARI, 2026

hatukufika kwenye hiyo shabaha ambayo tumepanga. Kwa hiyo hili ninadhani tukiweka hivyo katika sekta zote na tukazi-*manage* na tukazitungia sheria ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kwenye hizo shabaha tunaweza tukafika kule ambako tunatamani kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi uchumi wetu mwingi ni *informal*, upo kwenye sekta isiyokuwa rasmi, lakini kujenga uchumi wa kwenye *informal sector* ni kazi kubwa sana. Watanzania walio wengi sasa hivi wanafanya malipo, wanafanya *transaction* mbalimbali nje ya mfumo rasmi wa huduma za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuje na sera na kuisimamia. Mpango huu utupeleke hapo kuhakikisha kwamba sasa Watanzania wote wanaingia katika mfumo jumuishi wa masuala ya fedha ili *transaction* zote zipitie benki, zipitie kwenye simu na maeneo mengine katika mfumo ambao ni rasmi. Hapo tutaweza ku-*manage* vizuri uchumi wa nchi yetu na riba zitaweza kupungua kwa sababu sasa fedha zote zitakuwa zipo katika taasisi za fedha na tutakuwa tunazona hata zinavyo-*move* na kutembea zitaonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali iliyopo sasa hivi watu wana-*transact* kupitia cash, hatuwezi kujenga uchumi wa namna hiyo. Kwa hiyo, ninashauri Mheshimiwa Profesa hebu angalieni namna ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona nchi nyingi zimefanikiwa na Nchi ya India wamefanya hivyo. Tupunguze yale makato makubwa mtu anapotumia labda *M-pesa* au *Tigo pesa*; badala ya kukatwa zile *charges* zile zisiwe kubwa na ikiwezekana Serikali iweke ruzuku huku iziondoe kusudi watu wengi waweze kuvutiwa kufanya *transaction* kupitia katika mifumo iliyo rasmi. Pia benki iangaliwe ili zile *charges* zipungue na zikipungua nina imani Watanzania wengi wataweza kupitishia fedha zao katika eneo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ninalotaka kushauri ni suala la sekta binafsi. Nimefurahi sana katika mpango huu, tunasema 70% ya sekta binafsi ndiyo itakuwa inaongoza uchumi wetu. Hili ni zuri sana. Hata hivyo, ninataka kushauri kwamba hii sekta binafsi

5 FEBRUARI, 2026

tunayoisema basi Mheshimiwa Waziri tengeneza mfumo wa kuitambua hii sekta binafsi, tuwe na mfumo wa usajili ili wote tuwaone, tujue tunaposema sekta binafsi tunamsema nani? Bila kujali ukubwa, bila kujali udogo, hawa wote wapo huko wanachangia uchumi wetu, tuwaone. Kwa hiyo ukiwa na mfumo wa namna hiyo utatusaidia sana kuweza kujua namna ya kuweza kutekeleza na kusimamia hii sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano ninalotaka kulisema ni kwamba imefika mahali nchi yetu tunasifika kuwa na Muungano mzuri, (Muungano wa Tanganyika na Zanzibar). Huu ni Muungano mzuri na wa kuigwa, lakini hatuwezi tukawa wenyewe tukafika. Twende sasa, tuweke nguvu tulizokuwa nazo, tulizokuwa tunazitumia katika kuzikomboa nchi za Afrika, twende kwenye Jumuiya za Afrika, tuunganishe, tufike mahali tuunde *federation government* ya Afrika Mashariki na Afrika nzima. Afrika tukiungana tutaweza kujenga uchumi imara wa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tukienda kama Tanzania peke yetu, Wakenya wakaenda wenyewe, Waganda wakaenda wenyewe, hii ndoto ya kufikia kwenye uchumi mzuri itakuwa bado ni ngumu kwa sababu lazima sisi wenyewe tuweke mikakati ya kufanya biashara sisi wenyewe, ya ku-*share* rasilimali tulizonazo katika Bara la Afrika. Kwa hiyo, ninashauri sana *integration* ya Afrika nzima lazima tuiangalie na tuiwekee mikakati katika mipango hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la sita ninalotaka kushauri, lazima mpango huu utupeleke katika kuhakikisha tunakuwa na mfumo wa kutusaidia kwenda kulipa madeni ya watoa huduma na madeni ya wakandarasi. Sasa hivi wakandarasi wanadai fedha nyingi sana na Serikali imetekeleza miradi mingi. Yaani tumetekeleza miradi mingi sana kiasi kwamba sasa ile miradi wale wakandarasi wanadaiwa, wengine wanafilisiwa na benki, wengine wanashidwa kuwalipa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishindwa kuwalipa maana yake hawawezi kuwekeza, hatuwezi kuondokana na umaskini. Kwa hiyo hebu tuje na utaratibu wa kuona namna tutakavyowalipa hao

5 FEBRUARI, 2026

wakandarasi wa ndani, watoa huduma mbalimbali wa ndani ili zile fedha wakiwalipa zitachochea, zitaingizwa kwenye uchumi wetu, tutaweza kukua zaidi na uchumi utakua kwa kasi kubwa. Kwa hiyo hili ni la muhimu sana kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la saba ninalotaka kupendekeza kwa kifupi. Nchi yetu tunasifika kwa kuwa na ardhi kubwa, ardhi nzuri, ardhi yenye rutuba na yenye madini ya kila aina. Sasa, kazi kubwa ambayo tunatakiwa kuifanya ni kuwekeza rasilimali za kupanga, kupima na kumilikisha hii ardhi. Tukipanga na tukamilikisha Watanzania wakamiliki, hata tunapokwenda kwenye Muungano wa Afrika hatutakuwa na wasiwasi kwa sababu tunajua kwamba hii ardhi tayari inamilikiwa na sisi wenyewe. Sasa hivi kasi ya upimaji, kasi ya umilikishaji bado ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kusema ni hili mchango wa mashirika ya umma. Ninaipongeza sana Serikali imewekeza kwenye mashirika ya umma. Ninapochambua utaona karibu trilioni 86 zimewekezwa kwenye mashirika ya umma, lakini *calculate return on investment is less than 1%*, zile ambazo zinatokana na gawio. Kwa hiyo Serikali iweke mkakati namna sasa ya kuhakikisha zile fedha tulizoweka kwenye mashirika ya umma zilete mapato makubwa, zichangie katika uchumi mkubwa katika kutoa ajira na mambo mengine. Ninaamini hilo litakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, lakini la mwisho kabisa *integrated planning* waiangalie, itatupeleka mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu awabariki, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga. Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe ajiandae.

MHE. PASCHAL I. CHINYELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niungane na ndugu yangu Mheshimiwa Nape kumpongeza

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Rais wetu ambaye ni Mwenyekiti wa Chama kwa Chama kufikisha miaka 49 toka kuasisiwa kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na timu yake kwa kutuletea ripoti hii yenye matumaini makubwa sana kwa Watanzania. Katika hizi pongezi kwa Chama Cha Mapinduzi ninaomba nianzie hapo kwenye hoja yangu ya kwanza ya mafanikio ya Serikali ya CCM kwenye suala la barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote humu ni mashahidi, miaka ya kabla ya 2000 ndugu zetu hasa wa Kanda ya Ziwa Mikoa ya Mara, Mwanza na Shinyanga walikuwa wanakwenda katika safari zao kwa kutumia treni tu na wakati mwingine treni ikikorofisha walikuwa wanalala njiani. Vilevile, walipokuwa wana dharura ya kwenda kwao nyakati hizo ilitakiwa kusafiri kupitia Nairobi kwa watu wanaokwenda Mwanza na Shinyanga, inapita Nairobi, inapita Sirari mpaka Mwanza. Kwa hiyo, ilikuwa ni shida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wote tunashuhudia barabara ni nzuri, unatoka asubuhi unaingia Mwanza mchana. Pamoja na mafanikio hayo, ninaomba nipendekeze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara zinazotutoa Dar es Salaam na kwenye bandari zetu kwenda katika maeneo tuliyopeleka mizigo ikiwemo nchi za nje. Ninapendekeza katika mpango huu wa muda wa kati na muda mrefu tuanze kuwaza kutengeneza barabara nyingine kutoka Dodoma kuelekea mikoa ya Rukwa na Mbeya badala ya kutegemea tu barabara ya kupita Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara inayotoka Bihawana katika Jiji la Dodoma kupitia Vijiji vya Nkome, Chidilo mpaka Sanza. Kwa sasa ukifika pale Sanza unaelekea Manyoni, lakini ninapendekeza sasa ipasuliwe barabara kutoka Sanza ipite katika mapori ya Muhesi na Kizigo na kufika Rungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo barabara inayojengwa kutoka Itigi kupita Rungwa kwenda Makongorosi. Barabara hii ikitengenezwa

5 FEBRUARI, 2026

ikapasua, ikafika Rungwa maana yake ni kwamba ikishafika Rungwa itakatwa kwenda kushoto, itaingia Makongorosi, ikifika Makongorosi itakwenda Songwe kupitia Kilia Matundu, Mhyangaluo hadi Laela pale Sumbawanga Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivi tayari mizigo kutoka kwenye bandari zetu haitategemea tu njia ya Mbeya bali itapita katika njia hii ambayo kiukweli itakuwa ni fupi zaidi kuliko hizi njia nyingine ambazo tunazitumia. Kwa msingi huo mapato ya Serikali yataongezeka kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari ya mizigo pia yakipita yakafika Laela, maana yake ni kwamba yatavuka, yatapita Mwimbi yatakwenda kwenye mpaka mwingine ambao sasa tunaujengea barabara ya lami, mpaka wa Kasesha kuingia Zambia. Itakuwa inarahisisha na safari itakuwa ni fupi kuliko safari ya kupita Tunduma pekee ambako kama alivyosema mchangiaji mwingine foleni ni kubwa na inawapotezea muda sana wafanyabiashara. Kwa hiyo, ninaomba hilo Serikali katika kipindi hiki iangalie namna ya kuchukua hatua kama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalopenda kuchangia katika mpango huu wa maendeleo ni kuhusiana na suala la maji. Maji ni kila kitu katika maisha ya mwanadamu. Huwezi kuzungumzia maendeleo bila kuzungumzia maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto hapa Dodoma ya maji. Kila mtu anafahamu kwamba sasa Dodoma ni makao makuu ya nchi, lakini mipango na miundombinu ya maji iliyopo ni ya muda mrefu na ilikuwa ina-*suit population* ya wakati ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa Dodoma Mungu ametujalia tuna maji chini ya ardhi, lakini pia Mwenyezi Mungu ametujalia milima. Nilipata kufika Arusha nikashuhudia mradi ule mkubwa wa maji wa shilingi bilioni 500 ambao kwa kiasi kikubwa unategemea maji ya kisima na maji yale yamehifadhiwa kwenye matenki yaliyopo kwenye milima na yanashuka kirahisi sana kwa wateja.

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tenki moja maarufu ninalikumbuka lipo katika Kata ya Olmoti, watu wa Arusha wanafahamu. Tenki kubwa la zaidi ya lita 500,000 linashusha maji kwa watumiaji na wanayapata maji kwa ufanisi mkubwa sana. Sisi hapa Jiji la Dodoma tunazo Kata za Matumbulu, Mbabala na Mpunguzi, zina mlima na maji yapo chini. Tunaomba Serikali katika bajeti hii ijipange iweke utaratibu wa kujenga matenki katika milima na kuchimba visima ili ku-pump maji kwenye *reservoirs*, maji yaweze kushuka kwa watumiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma sasa hivi inajengeka kila kona, lakini upatikanaji wa maji bado ni ule wa zamani. Tunaomba na kushauri, matenki yajengwe kwenye bajeti zinazofuata ili watu waweze kupata maji kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ninaloomba kujadili hapa ni kuhusiana na migogoro ya ardhi. Hili hata Mheshimiwa Rais wakati anahutubia Bunge ukurasa wa 29 alisema yafuatayo: *“Tutaongeza kasi ya urasimishaji wa maeneo ya makazi na kuimarisha utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa kupima ardhi nchi nzima kwa teknolojia ya kisasa ya kisetelaiti (land geospatial technology)”*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Mkumbo pia katika taarifa yake ameelezea kuhusiana na suala la kuimarisha mipango miji na kupima viwanja. Wote sisi ni mashahidi, migogoro ya ardhi imetamalaki katika sehemu kubwa sana ya nchi na ninashukuru hata mwongeeji wa mwisho amelisema hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo shida kubwa sana hapa Dodoma ya migogoro ya ardhi. Katika mpango huu ninaomba sana Serikali ijikite katika kuangalia namna gani itashughulika na migogoro ya ardhi katika Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo katika hali ambayo watu waliomilikishwa ardhi mapema wanakuja kuondolewa na watu ambao wanazo hati tayari kwenye mikono yao. Leo hii nimepokea malalamiko ya watu karibu 10, wanazo *documents* za kumiliki ardhi walizopewa na CDA, lakini leo hii wanakwenda watu wenye *title deeds*, (wenye hati) wanawaondoa na ninafikiri wote mmeshuhudia

5 FEBRUARI, 2026

kule Mbuyuni, Kata ya Kizota watu wameenda kubomolewa nyumba zao wanaambiwa kwamba ardhi siyo ya kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hili tuliangalie kwa makini ili basi watu walio na haki ya kumiliki ardhi wamilikishwe wenyewe na wasimilikishwe watu wengine ambao hawahusiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho linaloungana na hili; Wilaya ya Dodoma Mjini ina watu zaidi ya 800,000 sasa na ina Mkuu wa Wilaya mmoja na Halmashauri moja ya Jiji la Dodoma. Katika kipindi hiki cha miaka 25 inayokuja ninaomba Serikali ifikirie kuigawa Dodoma katika halmashauri mbili, moja iitwe Mtumba lakini ninaomba nipendekeze halmashauri nyingine iitwe Halmashauri ya Mazengo ili tuwe na Jiji la Dodoma lakini tuwe na Manispaa mbili, Manispaa ya Mazengo na Manispaa ya Mtumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Mwanza walishafanikiwa, wana Halmashauri ya Ilemela, wana Manispaa ya Ilemela wana Manispaa ya Nyamagana. Dar es Salaam vilevile wana manispaa tano za Temeke, Kinondoni, Ilala, Kigamboni pamoja na Ubungo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii itawezesha upangaji mzuri wa maendeleo. Katika hili pia ambalo tunalisema la migogoro ya ardhi Serikali itaweza kulimudu vizuri kuliko ilivyo sasa ambapo Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa maoni yangu linatakiwa lisaidiwe kazi kwa kupewa manispaa mbili ambazo zitakuwa zinajitegemea. Halmashauri hizi zitapewa bajeti na kwa msingi huo zitatoa huduma njema, bora kwa wananchi wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Paschal Inyasi kwa mchango wako. Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Fadhili Sandali Chilombe na Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali ajiandae.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafsi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai,

5 FEBRUARI, 2026

lakini pili napenda nitumie nafasi hii pia kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuchangia Bungeni toka mwaka umeanza 2026, nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteua jina langu. Pia ninawashukuru wananchi wote wa Mkoa wa Katavi hususan akinamama kwa kunichagua tena kuwa mwakilishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Kitila Mkumbo na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Chaya alikuwa jirani yangu zamani hapa kwa kuleta mpango mzuri wa dira ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda sasa kwenye kuchangia, malengo ya Tanzania, ni kwamba ifikapo mwaka 2050, nchi hii iwe nchi ya hadhi ya kipato cha kati. Tunafikaje kwenye kipato cha kati? Tunafika kwenye kipato cha kati kwa kuhakikisha kwamba tunakuwa na viwanda vya kutosha nchini kwetu Tanzania, ili tuweze kuuza ndani ya nchi pamoja na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda nchini kwetu Tanzania vipo vinajengwa, lakini nchi hii sio kwamba inajenga viwanda kwa mara ya kwanza. Nchi hii ilikuwa na viwanda vya nguo kule MWATEX, MUTEX, URAFIKI, KILTEX, SUNGURATEX. Viwanda hivi vilikuwa vinatumia malighafi za pamba ambazo tulikuwa tunazalisha nchini kwetu Tanzania. Viwanda hivi sasa hivi havipo kwa sababu Serikali ilikuja na sera ya kubinafsisha viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali kwa kupitia Bunge hili, kama tuliweza kubinafsisha vile viwanda wakati ule tukawabinafsishia wananchi, lakini viwanda hivyo havifanyi kazi kwa sasa, Serikali ivichukue viwanda vile ili wananchi waweze kuuza pamba zao kwenye hivyo viwanda. *(Mkaofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuwa na viwanda vya nguo tu, tulikuwa pia na viwanda vya kutengeneza vitu mbalimbali. Tulikuwa na viwanda ambavyo vilikuwepo vinatengeneza mpaka nyama vinapeleka nje ya nchi, lakini tulikuwa na viwanda ambavyo vilikuwa vinatengeneza mafuta. Tukumbuke tu kwamba nchi hii ilikuwa na

5 FEBRUARI, 2026

viwanda takribani 364 ambavyo vilibinafsishwa. Ombi langu ni kuangalia ule ubinafsishaji ulikuwa na mkataba wa aina gani ili Serikali iweze kuvichukua viwanda hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kilimo. Tukiwekeza kwenye kilimo nchi yetu pia itaweza kusonga mbele; Lakini kwenye kilimo hiki wakulima wengi wamekuwa wakipata hasara wakati wanapouza mazao yao lakini na kutumia pesa nyingi kwenye kilimo hususan kwenye mbolea. Nichukue mfano zao la mahindi, mahindi wananchi wanapolima wanatumia mbolea, tuna uhaba wa mbolea nchini kwetu Tanzania, lakini kuna tatizo la mbegu ambazo zinapandwa za mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashindwa kuelewa kwa sababu tuna vyyo vyetu ambavyo vinafanyiwa *research* inakuwaje wananchi watumie mbegu ya mahindi wanapoipanda, wanaipanda mara moja, inapoota haiwezi kutumika tena. Ni kwa nini halifanyiwi *research* jambo hili? Wakati tuna chuo cha kilimo pale Morogoro, mbegu zinauzwa kwa gharama. Nichukulie mfano kule Katavi *packet* moja ya mbegu inauzwa mpaka shilingi 12,000, mfuko wa mbolea unauzwa kuanzia 75,000, lakini mbegu hii ya mahindi ili uweze kulima heka moja unahitaji *packet* tano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *packet* tano unazipanda unaweza ukavuna gunia 20, lakini katika zile gunia 20 huwezi kutenga gunia moja ili uweze kulitumia mwaka ujao kwa ajili ya mbegu. Ni kwa nini mbegu hizi haziwezi kupandwa tena kwa mara ya pili? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba watafiti wa kilimo watufanyie *research* hapa kuna tatizo, hapa kuna tatizo la mkulima kutumia pesa nyingi kwa kununua mbegu ambayo anaipanda mara moja, wakati mbegu zetu za asili unaweza kuvuna na ukaipanda tena mwaka unaofuata. Ninaomba liangaliwe hilo kwa manufaa ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la utalii nchini kwetu Tanzania. Utalii kama tulivyoongea filamu ya *Royal Tour* ambayo ilichezwa na Mheshimiwa

5 FEBRUARI, 2026

Rais iliongeza mapato ya utalii nchini kwetu Tanzania. Niiombe Serikali iwekeze kwenye miundombinu iliyoko kwenye hifadhi zetu nchini Tanzania, ili sasa tuweze kupata watalii wa kutosha kwa sababu utalii peke yake unaongeza pato la Taifa takribani 27%. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuizungumzia Mifuko inayolindwa *Ring Fenced Funds*. Kuna mifuko mitano ninaomba niitaje kwa haraka haraka; Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Maendeleo ya Reli, Mfuko wa Taifa wa Maji, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na Mfuko wa Maendeleo ya Utalii. Mifuko yote imeelekezwa kutoa asilimia tano kwa ajili ya maendeleo ya *EPZ*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni moja, fedha zinazokusanywa kwenye Mifuko hii huwa zinaangaliwa kivipi? Nikichukulia mfano Mfuko wa *TBL*, Mfuko wa Maendeleo ya Utalii Nchini Tanzania. Mifuko hiyo haina bodi ya kudhibiti fedha hizo. Ni ushauri wangu kwa sababu Mifuko hii imewekwa mahsusi kwa ajili ya maendeleo, lakini watu wanakatwa pesa wanachangia Mifuko hii, maana yake unapoweka mafuta, moja kwa moja unakuwa umechangia Mifuko hii. Hivyo basi, ningepomba utaratibu uwekwe mahsusi wa kuangalia pesa zinazotokana na mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ningeweza kulizungumza pia ni uboreshaji wa miundombinu ya barabara pamoja na reli. Kwenye Mkoa wangu wa Katavi, kwenye mpango uliopita mwaka 2020 kulikuwa na ujenzi wa reli ya *SGR* kutoka Kaliua, Mpanda mpaka Karema. Nimeona mpango huo umefutika. Ninaomba kujua na wananchi wa Katavi wanaomba kujua je, ule mpango wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* kutoka Kaliua, Mpanda mpaka Karema ambako tunakwenda kupokea mizigo kutoka Congo, Rwanda na Burundi na ambako Serikali imewekeza bandari kubwa kwenye Ziwa Tanganyika pale Karema, umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Restuta. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe, atafuatiwa na

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali na Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma ajiandae.

MHE. FADHILI S. CHILOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Ninaomba niungane na Wabunge wenzangu kuchangia hoja iliyo mbele yetu, lakini kabla sijachangia ninaomba nichukue fursa hii kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Tunduru Kusini na Tunduru kwa ujumla kwa changamoto kubwa ya umeme wanayopitia hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya umeme Tunduru ni mbaya na sababu ni kwamba hali ya hewa kule sasa hivi imekuwa ya tofauti kwa sababu mvua zinanyesha sana. Hata hivyo, ninataka niwape neno la matumaini, Serikali sikivu ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeshachukua hatua za awali kwa kupeleka timu ya TANESCO Mkoa wa Ruvuma wako pale wameanza kufanya kazi ya kumaliza zile kazi zao za mwisho ambazo zilikuwa ni muhimu kwao kuzifanya wakati wa ujenzi wa mradi unaoendelea kwenye eneo lile. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba, kazi ile itakapokamilika hili tatizo la umeme litakuwa limefika mwisho wa safari yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo kwa kazi nzuri aliyoifanya. Kazi ni nzuri na inatoa dira nzuri ya mwelekeo mzuri wa uchumi wetu. Mambo mengi yamesemwa kwenye maandiko yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka nichangie eneo dogo tu la sekta ya nishati kwa sababu watu wengi wameshachangia na waliochangia ni mambo mengi na ni mazuri zaidi. Hivyo, nitajikita kwenye nishati hasa ya umeme, ninataka nishauri huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza leo uwezo wetu wa kuzalisha umeme katika nchi ni *megawatt* 4,504 lakini ndani ya hii nchi uzoefu unaonesha kwamba, umeme unapotulia matumizi yanaongezeka. Hii maana yake ni nini? Kama nchi bado mahitaji ya umeme ni makubwa sana, lakini kazi ya kuhakikishia umeme kwenye maeneo hayo haijakamilika. Kwa hiyo, pale panapotulia na umeme ukafikishwa kwa sehemu, matumizi yanaongezeka.

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010 mpaka mwaka 2021 ukuaji wa umeme kwenye nchi hii ulikuwa asilimia 8.4 na mtakumbuka kwenye kipindi kile ndiyo kipindi ambacho nchi ilipita kwenye mgao mkubwa sana. Ilipofika 2022 kwenda 2025 matumizi ya umeme ukuaji uliongezeka kwa 13% kutoka kwenye 4.8 mpaka. Maana yake ni nini? Maana yake kwenye kipindi kile cha kutoka 2020 mpaka kufika 2025 ndiyo kipindi ambacho Julius Nyerere ilikuwa inaingiza mashine moja moja na kufanya upatikanaji wa umeme nchini kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto iko wapi? Iko shida sasa hivi Serikali inafanya jitihada kubwa sana ya kujenga hizo *line* kubwa kwa lengo la *ku-stabilize* wakati huo huo huku wanajenga *line* huku wanaongeza uzalishaji. Maana yake ni kwamba *demand* ya nchi itapanda. Kwa maana hiyo kama *demand* ya nchi itapanda maana yake Serikali lazima ijiandae kuhakikisha kwamba inaongeza uzalishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa nchi hii 67% unatokana na maji, 29% unatokana na gesi, asilimia 0.1 unatokana na jua, asilimia 2.5 unatokana na mafuta. Wote tunafahamu wakati tukielekea kwenye huo uchumi mkubwa unaoongelewa hapa ndani maana yake ni kwamba tunahitaji kuwa na umeme wa kutosha, lakini katika hali tuliyonayo sasa hivi wote tunajua kwamba nchi hii kama nilivyosema kiasi kikubwa cha umeme kinategemewa kutoka kwenye *hydro*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *hydro* inategemea maji na maji yenyewe ni mvua na mvua sasa hivi hakuna *consistency* kwenye upatikanaji wa mvua. Kuna mwaka mvua inapatikana, kuna mwaka haipatikani. Maana yake ni nini? Hapa ziko shida mbili moja ni hiyo ya uzalishaji kwa sababu kama nchi tukitegemea mvua peke yake, mwaka ambao mvua haitakuja tutarudi tena kwenye *crisis* ile ile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaamini kwamba kwa kuwa Julius Nyerere iko pale, basi changamoto ya umeme imekwisha kabisa, siyo sahihi. Hapa tunachotakiwa kufanya ushauri wangu ni kwamba Serikali iwekeze kwenye *solar*.

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Denmark wanaona jua wakati kwa kati ya masaa 1500 mpaka 1800 kwa mwaka, lakini wale watu wanazalisha umeme *gigawatt* 254.8 sawa na *megawatt* 254,800, lakini 15% ya umeme huo unatokana na jua. Sisi Tanzania tunaona jua kati kwa masaa kati ya 2,800 mpaka 3,500. Tafiti zinaonesha kwamba tukitumia jua letu vizuri tuna uwezo wa kupata mpaka *megawatt* 72.96.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yamekuwa yakishauriwa miaka yote Serikali haijachukua hatua inayotosheleza. Ninafahamu tumeanza Kishapu pale kwenye ule mradi wa kuzalisha *megawatt* 150. Mpaka sasa hivi katika kipindi chote hicho tumeshazalisha 50 pekee, ndiyo yale mambo alikuwa anasema Mbunge aliyetangulia pale kwamba tunafanya vitu polepole mno na tukienda kwa utaratibu huo wa kufanya maamuzi kwa pole pole, hili lengo halitatimia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa viongozi wenye dhamana tumsaidie Rais. Sisi kama Wabunge hapa ndani kazi yetu ni kushauri tu. Wale wenye dhamana wasaidie maono ya Rais yatimie na yanatimiaje? Yanatimia kwa kutekeleza, kwa kuthubutu na kufanya. Tukitumia umeme wa *solar* tukauzalisha kwa ukubwa wake maana yake kwamba tuwe *alternatives at a time*. Jua likikosekana ambalo haliwezi kukosekana, mvua ikikosekana umeme wa jua upo. Ukiwepo umeme wa jua tutakuwa na umeme wa mvua na wa jua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwa nchi kama ambayo muda wote tunalalamika mvua hazinyeshi, mvua hazinyeshi jua linawaka halafu hakuna umeme, hii kitu haiingii akilini. Ninawashauri viongozi kama kweli lengo letu ni kwenda kufika kwenye hilo lengo, lazima tutafute *alternative source* ya umeme. Hakuna uzalishaji, hakuna maendeleo yatakayopatikana kama hakuna umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hapo hapo kwenye umeme, watu wenye dhamana hapa tunaongelea habari za *megawatt* elfu nne mia nne na kitu. Hizi zinapatikana kwenye vyanzo vyote tunavyovifahamu kwa maana Mtera, Kihansi, Kidatu hivyo na kule mahali kuna mashine, zile mashine zina taratibu zake. Wale

5 FEBRUARI, 2026

wanaohusika na kazi hiyo wafanye kazi yao vizuri kuhakikisha kwamba mashine zipo *intact*. Hapa leo Bwawa la Mtera likienda *down* kwa maana ya mashine zimeharibika hizi 4,000 hazipo. Tutakuwa tunazitamka tu kwamba tuna *installed capacity* lakini *available* siyo hiyo. Tutaingia kwenye *crisis* nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo pia la kuziangalia hizi mashine zipate mazingira yake yaliyo sawasawa ili tuhakikishe kwamba haya mambo tunayoongea yanatimia. Wakati ninaelekea kumalizia mchango wangu, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa dhati ya moyo wangu. Mimi ni mgeni mpya hapa ndani, ni Mbunge Mpya, nilikwenda pale kumweleza changamoto ya jimboni kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimboni kwetu kuna changamoto kubwa na siyo jimbo *actually* ni wilaya nzima ina changamoto kubwa sana ya migogoro ya wafugaji na wakulima. Watu wanakufa kule, wafugaji ni wababe. Mfugaji anakuja anamwambia mkulima ninakupa siku nne uvune mpunga wako, usipovuna ninaingiza ng'ombe. Asipovuna kweli anaingiza ng'ombe, akijitetea anamchoma mkuki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemweleza Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninamshukuru sana, popote alipo asikie amechukua hatua amewaagiza Mawaziri wawili: Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na Waziri wa TAMISEMI. Wameniahidi kwamba baada ya Bunge hili watakuja Tunduru kuja kutafuta suluhu ya jambo hili. Sasa namna hii jinsi wanavyo-act Mawaziri, tu-act na kwenye Mpango ili tufike. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Fadhili ahsante sana. Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma na Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya ajiandae.

5 FEBRUARI, 2026

(Hapa Mhe. Nassriya Nassir Ali alichangia kupitia mtaalamu wa lugha ya alama)

MHE. NASSRIYA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, lakini kabla ninaomba uniruhusu nizungumze nikiwa nimekaa kwa sababu ninatua lugha ya alama. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Keti, ahsante.

MHE. NASSRIYA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kama nilivyosema ninashukuru kwa fursa ambayo umenipa. Pia, nimshukuru Mungu kwa kunipa afya njema kwa kuwepo hapa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana pia Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu. Mimi ni mtu mwenye ulemavu, ninakishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi kwa imani yao kwangu nikiwa Mbunge wa kwanza kiziwi hapa Tanzania tangu Bunge hili kuanzishwa. Ninamshukuru sana Rais kwa kuweza kuvunja huu mwiko na kuwepo kwa Mbunge kiziwi Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila ninaomba nimshukuru mama yangu kwa kazi kubwa sana ambayo ameifanya ya kunilea mpaka kufika mahali hapa. Ninamwomba sana Mungu ambariki. Mama yangu amekuwa ni Balozi wa watu wenye ulemavu, ninamshukuru sana, sana mama yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru pia kwa fursa hii. Ninaomba pia nimshukuru Mheshimiwa Profesa Mkumbo Waziri wa Wizara ya Mipango na Uwekezaji, kwa namna ambavyo alitushirikisha katika kukusanya maoni na hatimaye maoni yetu yote yamezingatiwa. Ninamshukuru sana Profesa amefanya kazi kubwa sana, kiukweli tumeridhika na wenzangu wenye ulemavu pia wamenituma nimshukuru amefanya kazi kubwa tumeridhika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie kwenye maeneo matatu. Kwanza eneo la elimu, afya na ajira. Nianze na elimu.

5 FEBRUARI, 2026

Ninaomba Serikali tunakoelekea iweze kuongeza shule za watoto wenye ulemavu kuanzia shule za msingi kwenye ngazi ya wilaya mpaka mkoa. Kwa sababu shule za wenye ulemavu zipo chache sana, kwa hiyo watoto wenye ulemavu wanapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi binafsi shule ya msingi nimesoma Dar es Salaam lakini nilitoka Zanzibar, pia Sekondari ilinilazimu kwenda Njombe, kwa hiyo ilikuwa ni changamoto kubwa. Ninamshukuru Mungu alinifanikisha nikamaliza kidato cha nne, kwa hiyo ninaiomba Serikali iweze kuongeza shule za watoto wenye ulemavu kuanzia ngazi ya wilaya mpaka mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba vile vile Serikali iweze kuongeza walimu wa elimu maalum ambao wana ujuzi wa kutosha kuwafundisha watoto wenye ulemavu, hapo tutaweza kufanikisha vizuri malengo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba shule hizi ambazo zitajengwa, ninaomba ziwe shule za *boarding*. Kwa kuwa wazazi wengi wenye watoto wenye ulemavu uwezo wao ni mdogo, kwa hiyo wakiwa wanalala bweni angalau itapunguza makali ya maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya; kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa jitihada kubwa sana katika kuboresha miundombinu. Hata hivyo, ninaomba niongeze kidogo, niionbe Serikali iboresha zaidi miundombinu. Kwenye vituo vya afya kuwe na wakalimani ikitokea mtu ambaye ni kiziwi anaumwa kawaida binafsi huwa sipendi kutumia mkalimani kwa sababu ya usiri wa changamoto zangu za kiafya. Kwa hiyo, pendekezo langu ningependa pia watoa huduma wa afya wapewe mafunzo ya lugha ya alama ili kuweza kurahisisha mawasiliano na kuwa na usiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa miundombinu hasahasa vitanda vya akina wajawazito wanapoenda kujifungua. Vitanda vingi ni virefu viko juu, kwa hiyo ningependekeza waboresha vitanda viwe vya chini kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Pia, niombe na niombe sana Serikali, iruhusu kurekebisha kanuni kidogo kwa

5 FEBRUARI, 2026

upande wa wanawake wenye ulemavu, wasioona wanapokwenda hospitali kwa ajili ya uzazi iruhusu waweze kuingia na ndugu zao. Kwa sababu tuna kisa kimoja, kuna mama mmoja sasa hivi ni marehemu alijifungua watoto mapacha, lakini kwa bahati mbaya aliibiwa mtoto mmoja akabakiwa na mtoto mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningepomba sana Serikali iruhusu hilo ili akina wajawazito wasioona wanapoenda kujifungua wawe na ndugu zao waweze kuwaangalizia watoto. Tulipata shida sana kufuatilia hiyo kesi, lakini basi mwisho wa siku alibaki na huyo mtoto mmoja. Kwa hiyo, ninaomba sana ombi hilo liweze kuchukuliwa na liweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa ajira. Kuhusu ajira wapo wazazi wenye ulemavu wamepambana sana kuwasomesha watoto wao na watoto wao wamefika mpaka ngazi ya *degree*, lakini wanapokuja mtaani hawana ajira. Kwa hiyo, ningepomba sana watoto ambao wamezaliwa na wazazi ambao wana ulemavu wapewe kipaumbele cha ajira ili waweze kuwasaidia wazazi wao ambao ni ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mkoa wa Iringa wamekuwa ni mfano wa kuigwa. Pale mjini kuna kituo cha watu wenye ulemavu ambao wanafanya kazi mbalimbali kama: useremala; ushonaji; na shughuli nyingine. Kwa hiyo, kimekuwa ni kituo muhimu kwa ajili ya ajira. Kwa hiyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Iringa, lakini pia niwashukuru Wabunge. Ninaomba tuige mfano wa Mkoa wa Iringa. Kile kituo kinaitwa *Neema Craft*, kimefanya watu wenye ulemavu wasihangaika mtaani, wengi wamechukuliwa pale wanafanya kazi na imekuwa ni fursa kwao ya ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nirudi nyuma kidogo kwenye upande wa afya. Sisi watu wenye ulemavu tuko makundi tofautitofauti na tuna vyama 12 vinavyowakilisha watu wenye ulemavu. Kuna wenzetu wenye ulemavu wa afya ya akili ambao wanatumia dawa ili angalau maisha yaweze kuwa mazuri. Kwa hiyo ningepomba dawa zao angalau gharama ipunguzwe. Pia kuna wenzetu wenye ulemavu wa ngozi (*psoriasis*). Ngozi yao inakuwa ibababuka na mafuta yao na

5 FEBRUARI, 2026

dawa zao ni gharama sana. Kwa hiyo, ningepomba pia gharama kwenye dawa zao zipunguzwe ama wapewe bure kwa ruzuku kama ambavyo ipo kwenye dawa za ARV kwa ajili ya HIV watu wanapewa bure na wao iwe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nimshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa kumchagua Mheshimiwa Ummy kuwa Waziri. Tunatoka wote Unguja anafahamu mambo mengi na anaendelea vizuri sana katika kusimamia masuala ya watu wenye ulemavu na aendelee hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali kwa mchango wako mzuri, tunakushukuru sana.

Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI: Bunge linarejea.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninaomba nimpishe Mheshimiwa Spika aendelee na ratiba inayofuata.

Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

SPIKA: Katibu.

5 FEBRUARI, 2026

NDG. JOSHUA CHAMWELA, ndc – KATIBU MEZANI:

**MATOKEO YA UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE
TAASISI MBALIMBALI**

NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha matokeo ya uchaguzi ambao umefanyika leo kwa nafasi mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze na Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge, nafasi saba. Idadi ya kura zilizopigwa ilikuwa ni 301.

Ninaomba kuanza na kundi A Wabunge kutoka Chama Tawala nafasi tano; Tanzania Bara wanaume nafasi mbili:-

- (1) Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, idadi ya kura 296;
- (2) Mheshimiwa Dkt. Mahera Charles, idadi ya kura 263;
- (3) Mheshimiwa Patali Shida Patali, kura 17; na
- (4) Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, kura 19.

Mheshimiwa Spika, Tanzania Bara wanawake nafasi moja:-

- (1) Mheshimiwa Dkt. Catherine Canute Joachim, kura 289; na
- (2) Mheshimiwa Asha Salum Motto, kura nane.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar wanaume nafasi moja: -

- (1) Mheshimiwa Haji Amour Haji, kura 280; na
- (2) Mheshimiwa Amjadi Ussi Salum Pondeza, kura 11.

Mheshimiwa Spika, Zanzibar wanawake nafasi moja:-

5 FEBRUARI, 2026

- (1) Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, kura 263; na
- (2) Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, kura 28.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Kambi ya Walio Wachache nafasi mbili:-

- (1) Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, kura 294; na
- (2) Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, kura 290.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, waliochaguliwa Tanzania Bara wanaume nafasi mbili ni Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko; na Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera Charles. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania Bara wanawake nafasi moja: Mheshimiwa Dkt. Catherine Canute Joachim. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Zanzibar wanaume nafasi moja: Mheshimiwa Haji Amour Haji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Zanzibar wanawake nafasi moja: Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Walio Wachache nafasi mbili: Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza; na Mheshimiwa Ado Shaibu Ado.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Bunge wa Afrika (*PAP*). Idadi ya kura zilizopigwa ni 301: Kundi A Wabunge wanawake:-

- (1) Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha, kura 290; na
- (2) Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, kura saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi B, Wabunge Zanzibar nafasi moja:-

- (1) Mheshimiwa Imamu Mtumwa Vuai, kura 289; na

5 FEBRUARI, 2026

(2) Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid, kura nane.

Mheshimiwa Spika, kundi C, Wabunge Tanzania Bara nafasi mbili:-

(1) Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula, kura 280;

(2) Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari kura 280;

(3) Mheshimiwa Thomas Mgonto Kitima kura sita; na

(4) Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, kura 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Walio Wachache; Mheshimiwa Rashid Habib Ali, kura 277.

Mheshimiwa Spika, hivyo, waliochaguliwa Wabunge wanawake nafasi moja: Mheshimiwa Lulu Guyo Mwacha; na Wabunge toka Zanzibar ni Mheshimiwa Imamu Mtumwa Vuai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge Tanzania Bara nafasi mbili: Mheshimiwa Mariam Anzuruni Mungula; na Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge Kambi ya Walio Wachache, Mheshimiwa Rashid Habib Ali.

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu, Wabunge wa Jukwaa la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC-PF)*. Idadi ya kura 301, Wabunge wanawake nafasi moja: Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, huyu ameingia kwa nafasi yake ile ya Mwenyekiti wa *TWPG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi B, Wabunge Zanzibar nafasi moja:-

(1) Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, kura 282; na

(2) Mheshimiwa Ali Haidar Madeweyya, kura 16.

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Spika, kundi C, Wabunge wa Tanzania Bara nafasi mbili: -

- (1) Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba, kura 270;
- (2) Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda, kura 290;
- (3) Mheshimiwa Ali Mchungahela, kura 25; na
- (4) Mheshimiwa Josephine Joseph Kapoma, kura 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi D, Wabunge Walio Wachache nafasi moja: Mheshimiwa Mohamed Khalfan Issa, kura 248. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochaguliwa: kwa Wabunge wanawake ni Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Zanzibar nafasi moja: Mheshimiwa Kassim Hassan Haji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge Tanzania Bara nafasi mbili: Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda; na Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Walio Wachache moja Mheshimiwa Mohamed Khalfan Issa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kundi la Nne, Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Idadi ya kura ni 301: Kundi A - Wabunge Wanawake:-

- (1) Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana kura 283; na
- (2) Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge kura 18.

Mheshimiwa Spika, kundi B – Wabunge Zanzibar, nafasi moja:-

- (1) Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid kura 284; na

5 FEBRUARI, 2026

(2) Mheshimiwa Yumna Mmanga Omar kura nane.

Mheshimiwa Spika, kundi C – Wabunge wa Tanzania Bara, nafasi nne:-

- (1) Mheshimiwa Mhandisi Fatma Ally Rembo kura 276;
- (2) Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu kura 285;
- (3) Mheshimiwa Asha Juma Feruz kura 267;
- (4) Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi kura 290;
- (5) Mheshimiwa Emmanuel John Khambay kura moja (1);
- (6) Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas kura 17;
- (7) Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda kura 20; na
- (8) Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume kura tano (5). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi D – Wabunge wa Kambi ya Walio Wachache; Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye kura 251.

Mheshimiwa Spika, waliochaguliwa; Wabunge Wanawake nafasi moja, Mheshimiwa Dkt. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana.

Mheshimiwa Spika, Wabunge Zanzibar nafasi moja, Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid.

Wabunge Tanzania Bara nafasi nne, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, Mheshimiwa Asha Juma Feruz na Mheshimiwa Mhandisi Fatma Ally Rembo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Walio Wachache nafasi moja, Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye. *(Makofi)*

5 FEBRUARI, 2026

Jukwaa la Kibunge la Nchi za Maziwa Makuu. Idadi ya kura zilizopigwa ni 301. Wabunge Wanawake nafasi moja:-

- (1) Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula kura 286;
- (2) Mheshimiwa Magreth Baraka Ezekiel kura 15.

Mheshimiwa Spika, Wabunge Zanzibar nafasi moja:-

- (1) Mheshimiwa Saidi Salim Hamad kura 274; na
- (2) Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis kura 15.

Mheshimiwa Spika, Wabunge Tanzania Bara nafasi mbili:-

- (1) Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa 285;
- (2) Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala 255;
- (3) Mheshimiwa Festo Richard Sanga 33; na
- (4) Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle kura 22.

Wabunge Kambi ya Wachache nafasi moja; Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo 242. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochaguliwa ni; Wabunge Wanawake nafasi moja; Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Zanzibar nafasi moja; Mheshimiwa Saidi Salim Hamad.

Mheshimiwa Spika, Wabunge Tanzania Bara nafasi mbili; Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa; na Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Walio Wachache; Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo. (*Makofi*)

5 FEBRUARI, 2026

Mheshimiwa Spika, matokeo haya yamethibitishwa na mashahidi kwa kuweka saini zao kwenye karatasi hii. Ninaomba kuwasilisha.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuomba Mwongozo wa Kiti kuhusiana na jambo lililotokea mapema leo wakati tukifanya zoezi la kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo yako, mwanzoni ulisema nafasi hizi zinaombwa na watu wanaoweza kuongea Kiingereza, lakini wakati zoezi hili likiendelea tumeshuhudia mwombaji mmoja, ambaye amechaguliwa kuwa mwakilishi wa nchi yetu kutoka Kambi ya Walio Wachache, sijamjua jina vizuri, nimesikia anaitwa Mheshimiwa Shingo; umeshuhudia mwenyewe ameshindwa kujieleza Kiingereza, hata cha kwangu kina nafuu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa maelezo yako, ninataka kupata Mwongozo kwamba na aliomba kwa Kiswahili, kama inaruhusiwa kupeleka watu wenye Kiswahili, kwa nini mnatunyima nafasi ambao hatukupata bahati ya kujua Kiingereza na yeye kwa nini aende? Ninashukuru na ninaomba Mwongozo wako? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Musukuma ameomba Mwongozo. Hili ni jambo la nini tu, hii ni demokrasia na *this time* tumechaguana, siku zote tuna-*nominate* haya majina na Kambi ya Upinzani wako wachache, nafasi iliyokuwepo ya nafasi ya Kambi ya Upinzani ni nafasi moja tu, hakuwa na mshindani kwenye nafasi hiyo.

Sauti ya wengi, ninyi ndio mliomchagua, labda wewe hukumchagua, lakini wenzako wamemchagua. Wamemchagua, kura zimepigwa wazi, zimehesabiwa wazi na mawakala wamesaini karatasi zote kuthibitisha wamehakiki kuchaguliwa kwa ndugu yetu huyu. *(Makofi)*

Huko atakapokwenda atajifundisha Kiingereza na ataelewa. Tunapopeleka watu siyo lazima hao wote wanakwenda kuchangia, lakini kuna misimamo ya nchi na nchi, lazima tupige kura kwa

5 FEBRUARI, 2026

misimamo ya nchi ambazo ni marafiki na wao wanataka kuingia kwenye nafasi hizi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Musukuma kwa bahati mbaya labda hukujua masharti haya, lakini masharti haya yanakwenda na busara na hekima. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ninawapongeza leo tumefanya demokrasia ya haki. Tumepiga kura kwa uwazi, zimehesabiwa kwa uwazi na zimethibitishwa kwa uwazi. Bado tunazo nafasi za uteuzi.

Kuna Chama cha CPA (*Commonwealth Parliamentary Association*), nimeshauri tusitangaze leo; tuna APC (*African Pacific Caribbean*), ni vyama muhimu sana. Tuna *Friendship Group* ya UAE, tuna *Friendship Group* ya Saudia na tuna *Friendship Group* ya Qatar; tuna *Friendship Group* ya Kuwait, tuna *Friendship Group* ya Morocco, tuna *Friendship Group* ya Canada, Uingereza na Serbia, zote hizi zinataka undugu na sisi na zote hizi ni nafasi. Hawa watakaokwenda huko hatutawachanganya na hao ambao wameshinda, hakuna mtu atakayeingia kwenye nafasi mbili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutapata hizi nafasi. Tunazo *training* za Wabunge ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi wale ambao kura hazikutimia, kuna mambo mazuri yanakuja kwenye Bunge hili.

Ninawapongeza wale walioshinda, mjue mnakwenda kutuwakilisha kwenye mataifa ya nje. Nidhamu na heshima kwa nchi yetu ni kitu cha kwanza, hicho ni kitu muhimu sana. Mheshimiwa Kingu ulikuwa unamwona kabla ya matokeo anakaa anasali; sasa Mheshimiwa Kingu unasali kabla kura kupigwa. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, hongereni sana. Tumemwona Katibu wetu wa chama, Mheshimiwa Shangazi, ndiyo kuishi na watu vizuri. Ukijenga mahusiano na watu, katika nafasi hizi unakwenda. Kwa hiyo, ninawashukuru sana. Baada ya maneno haya ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.28 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 6 Februari, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*